

الْحَمْدُ لِلَّهِ وَالْمِنَّةُ

*Kitabu hiki ni Jibu la kitabu 'Yanaabii UI Islam'  
cha Mkristo mmoja, kiitwacho*

**CHEMCEM**

**YA**

**UKRISTO**

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad<sup>as</sup>  
Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu  
Waa hmadiyya

Mfasiri

Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya

**JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA  
TANZANIA**

## **CHEMCHEM YA UKRISTO**

Tafsiri ya Kiswahili ya: Chashma e Masihi (Urdu)

Mfasiri: Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya

Sura ya nje: Sharifu Tanwir Mujtaba

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): Qadian 1906

Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2011

Nakala: 2000

Kimeenezwa na:

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania

Mtaa wa Bibi Titi Mohamed

S.L.P. 376, Dar es Salam.

Simu: +255222110473

Fax: +255222121744

Kimechapwa na:

Ahmadiyya Printing Press

Dar es Salam, Tanzania

Simu: +255222111031

ISBN: 978-1-84880-533-0

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ<sup>1</sup>  
نُحَمِّدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ<sup>2</sup>

## MAELEZO YA MWENEZI

### KUHUSU MWANDISHI

Mwandishi wa kitabu hiki Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyehadiwa na Imam Mahdi a.s. alizaliwa tarehe 13 February 1835 huko Qadian, India. Alijitolea maisha yake yote kujifunza elimu ya Kurani Tukufu na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Kwa kuona hali duni ya Waislamu na kushambuliwa sana na wapinzani, alimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu sana kwa ajili ya mafanikio ya Islam. Vile vile alikubali kujibu shutuma za wapinzani na kutetea dini ya kweli. Mwenyezi Mungu Alimchagua kuwa Imamu wa zama hizi. Hivyo aliielezea dunia mafundisho sahihi ya Islam. Kwa kupata lengo hili aliandika vitabu zaidi ya 80 katika lugha ya Kiurdu na Kiarabu. Kwa njia ya kutoa hotuba na kufanya mijadala na viongozi wa dini zingine

---

<sup>1</sup> Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

<sup>2</sup> Tunamhimidia yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

alifanya kazi ya maana sana ya kueneza na kutetea Kitabu cha Mungu. Alithibitisha kwamba Islam pekee ndiyo dini illiyo sahihi na hai siku hizi inayoweza kujenga na kuimarisha uhusiano kati ya mtu na Mwumba wake. Alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu Amemchagua kuwa Imam Mahdi na Masihi Aliyehidiwa, sawa na bishara za Biblia, Kurani na Hadithi za Mtume saw. Sawa na amri ya Mwenyezi Mungu alianzisha Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah tarehe 23 Machi 1889 huko Ludhiana, India. Sasa Jumuiya yake inapatikana katika nchi 197 za dunia. Baada ya yeye kufariki, Mwenyezi Mungu Alianzisha nidhamu ya Ukhalifa katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah kuendeleza shughuli zake. Siku hizi Khalifa na Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah ndiye Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a.

### KUHUSU KITABU

Naona furaha kuweka mbele ya wasomaji tafsiri hii ya kitabu cha Seyyidna Ahmad a.s., Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, kiitwacho “*Chashmae Masihi*” (chemchem ya Ukristo) kilichochapishwa mnamo

## Chemchem ya Ukristo

---

Machi 1906. Kitabu hiki kinajibu kitabu maarufu cha Wakristo “*Yanabiul- Islam*” (chemchem za Islam) kilichoshutumu kwamba Kurani haifundishi lolote jipia, bali imenukuu tu vitabu vya zamani.

Seyyidna Ahamad a.s. akijibu ameandika kwamba Mayahudi wamethibitsha kwamba Injili imenukuliwa neno kwa neno kutoka Talmudi, na Wahindu wamesema kwamba Injili imenukuliwa kutoka katika vitabu vya Kibudha, na Watafiti walio Wakristo wameandika kwamba ibara za Injili zinafanana sana na kitabu cha Yuz Asif.

Seyyidna Ahamad a.s. ameandika kwamba kama mafundisho ya Kurani yanafanana kidogo na vitabu vya zamani, hiyo ni kwa sababu ya wahyi kutoka kwa Mungu, waila Mtume Mtukufu s.a.w. ambaye hakujua kusoma hata Kiarabu alijuaje Kigriki au Kiebrania.

Baada ya kueleza ufasaha wa pekee wa Kurani Tukufu amebatilisha itikadi za Wakristo kama vile Utatu, Uungu wa Yesu na Kafara yake. Vile vile ameeleza mafundisho ya Islamu na Ukristo kuhusu kusamehe na kisasi. Mwishoni ameandika hakika ya wokovu.

## SHUKRANI

Kitabu hiki kimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya, Mbashiri wa Tanzania.

Katika Makao Makuu katika *deski ya Kiswahili* Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Tanzania na Kenya na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Tanzania waliichunguza tafsiri hii kwa kuilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu sana na kuidurusu.

Aidha ndugu kadhaa wengine nao wakasaidia kwa njia mbalimbali, kama vile Sheikh Ansar Hussain, Sharifu Tanwir Mujtaba na Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin.

Chaudhry Muhammad 'Ali M.A.

Wakilut Tasnif

Tahrik e Jadid

Rabwah. Pakistan

12 Julai, 2011

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ<sup>3</sup>  
نَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ<sup>4</sup>

## TANGAZO KUTOKA KWANGU LINALOELEZA BISHARA ZA TETEMEKO

*Marafiki! zindukeni, tetemeko laja tena.  
Mungu yuko tayari tena kuonyesha haraka  
nguvu yake.*

*Tetemeko mlilolishuhudia mwezi Februari,  
muwe na yakini kuwa hilo lilikuwa ni onyo  
tu kwa kutahadharisha.*

*Itibuni kwa kutiririsha machozi, enyi  
mlioghafilika, sasa mbingu i karibu  
kuporomosha moto.*

*Kwa nini yasije matetemeko, ilhali njia ya  
Ucha Mungu imepotea. Hata Mwislamu  
ndio Mwislamu wa jina tu.*

*Nani aliyenikubali kwa kuogopa na nani  
akaacha bughudha na chuki! Maisha  
yangu ndiyo kwa kutukanwa tu.*

---

<sup>3</sup> Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

<sup>4</sup> Tunamhimidia yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

## Chemchem ya Ukristo

---

*Wote waniita kafiri na dajjali na fasiki.  
Nani ndiye aaminiye kwa ukweli na  
uaminifu!*

*Kila umwonaye, ameruka mipaka kudhania  
vibaya. Kama mtu akimwuliza (Kunihusu),  
aeleza mamia ya aibu (zangu).*

*Wanaiacha dini na kuipenda dunia. Hata  
nikitoa mawaidha na nasaha mara mia,  
nani ndiye ajutaye!*

*Kwa kuona msiba wa dini, moyo  
unahangaika. Lakini mkono wa Mungu  
ndio uutulizao sasa.*

*Hivyo, sasa, ghera yake itawaonyesheni  
kitu. Afa hili li karibu kunyosha mkono  
wake kila upande.*

*Kwa njia ya mauti, sasa, dini itapata  
msaada; la sivyo, dini itakufa siku moja.*

*Kulikuwa na wakati dunia nzima  
ilipojitolea kwake, lakini siku zimefika  
ambapo hata mtu duni kabisa naye  
anaikadhibisha dini hii.*

Mtangazaji,

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,

Masihi Mau'udi.

9 Machi 1906



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ<sup>5</sup>  
نُحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ<sup>6</sup>

## CHEMCHEM YA UKRISTO<sup>7</sup>

Kitabu nilichokiita 'Chemchem ya Ukristo' kwenye kichwa cha habari kwa hakika ndicho kitabu hiki tutakachoandikia hapa chini. Sisi hatukuwa na haja ya kuandika chochote juu ya itikadi za Mapadri, maana, siku hizi wakuu wao watafiti wa Ulaya na Amerika wameshika mkononi mwao kazi hii tuliyopaswa kuifanya, na wanatoa huduma hii vizuri sana ya kubainisha kuwa dini ya Kikristo ni kitu gani na hakika yake ni nini. Laikini siku hizi barua moja ya Mwislamu mmoja nisiyemjua imeniwasilia kutoka Bans Bareli. Katika barua yake ameeleza madhara ya

---

<sup>5</sup> Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

<sup>6</sup> Tunamhimidia yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

<sup>7</sup> Jina hili halimaanishi kwamba hii ni chemchemi ya Yesu, kwani mafundisho ya Bwana Yesu yaliyopotea duniani hayakufundisha itikadi hizi zilizopo, bali haya ni mafundisho yaliyozushwa na Wakristo wenyewe. Hivyo, kitabu hiki kimepewa jina la 'Chemchemi ya Ukristo'.

kuogofya ya kitabu cha *'Yanaabiul Islam'* ambacho ni kitabu cha Mkristo mmoja. Inasikitisha kuwa Waislamu wengi kwa sababu ya mghafala wao, hawavisomi vitabu vyetu, na wala hawana habari ya baraka za Mwenyezi Mungu Alizotuteremshia. Na masheikh wajinga kwa kukariri kutuita makafiri wamejenga ukuta baina yetu na Waislam wengine wa kawaida. Watu hao hawajui kuwa zimekwisha pita zama ambapo hila na ulaghai wa Kikristo ulikuwa unafanya kazi kidogo. Na sasa ndio mwishomwisho wa mwaka wa elfu sita tangu Adam azaliwe ambamo silsila ya Mungu itapata ushindi. Na ndiyo vita<sup>8</sup> ya mwisho baina ya nuru na giza, ambamo nuru itapata kushinda na kusaidiwa, na giza litafikia mwisho wake. Na hakukuwa na haja ya kuandika chochote juu ya mawazo mabovu ya mapadre, lakini kwa sababu ya kusisitiza kwa mtu mmoja

---

<sup>8</sup> Kwa neno hili la vita isifikiriwe kuwa vita hivi vitapiganwa kwa upanga na bunduki, kwani Mwenyezi Mungu Amekataza sasa jihadi ya aina hii. Maana, ililazimu kuwa katika zama za Masihi aliyeahidiwa jihadi ya aina hii ikatazwe kama Kurnai Tukufu ilivyokwisha toa habari hii hapo awali, na ndani ya Sahihi Bukhari kumhusu Masihi aliyeahidiwa mna Hadithi inayosema kuwa: *يَصْعُ الْحَرْبُ* (Yaani atakomesha vita). Mwandishi.

aliyetajwa hapo juu imebidi kuandika kijitabu hiki. Mwenyezi Mungu Akitilie baraka na Akijalie kiwe sababu ya watu kupata mwongozo. Amin.

Na ikumbukwe kuwa sisi tunamheshimu Bwana Yesu na tunamwamini kuwa Nabii wa Mwenyezi Mungu.<sup>9</sup> Nasi tunapinga shutuma za Mayahudi zilizoenezwa siku hizi. Lakini sisi tunataka kuonyesha kuwa kama ambavyo kwa sababu ya chuki zao Mayahudi wanamshambulia Yesu na Injili yake, ndivyo hivyo Wakristo wanavyoishambulia Kurani Tukufu na Mtume s.a.w. Haikuwapasa Wakristo kuwafuata Mayahudi katika njia hii mbovu. Lakini ndiyo kawaida kuwa mtu asipoweza kuishambulia dini fulani kwa njia ya haki na uadilifu, hapo watu wengi huanza kufanya mashambulizi kwa njia ya masingizio ya uwongo. Basi, ndiyo ya aina hiyo mashambulizi ya mwandishi wa “Yanabiul Islam”. Mazoea haya mabaya yanasababishwa na

---

<sup>9</sup> Yoyote iliyoyaandika kalamu yetu dhidi ya shani ya Bwana Yesu ndiyo kwa kuwasuta kwa sababu ya mashambulizi yao, nayo ndiyo kwa kweli maneno ya Mayahudi ambayo tumeyanakili. Ole wao! Kama mapadri watumie uungwana na ucha-Mungu, na wasimtukane Mtume wetu s.a.w., basi hapo upande wa pili Waislam nao wataonyesha adabu mara ishirini zaidi kuliko hao. Mwandishi.

## Chemchem ya Ukristo

---

huba ya dunia; waila katika zama hizi dini ya kimbingu ni Islam tu ambayo baraka zake mpya mpya zinapatikana. Na hii ndiyo baraka ya chemchemi ya Islam tu kwamba hiyo inamfikisha mtu kwa Mwenyezi Mungu Aliye Hai; waila yule mungu wa bandia aliyezikwa Sri Nagar (mtaa wa Khanyar) Kashmir, hawezi kumsaidia mtu.

Sasa tunamwelekea bwana huyu mwandishi kutoka Bareli na tunahariri kijitabu chetu hiki. Na Mungu ndiye Awezashaye.

Mwandishi,  
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,  
Masihi Mau'ud  
1 Marchi 1906

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ<sup>10</sup>  
نُحَمِّدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ وَنَبِيِّهِ الْعَظِيمِ<sup>11</sup>

Assalaamu Alaikum! Baada ya hii ibainike kuwa nimesoma kwa masikitiko makubwa barua yako, uliyoandika baada ya kusoma kitabu cha Mkristo mmoja kiitwacho “Yanaabiul Islam”. Mimi nastajabu kuwa watu ambao mungu wao ni mfu, ambao dini yao imekufa ambao kitabu chao ni kifu, na ambao wenyewe ni wafu kwa kukosa jicho la kiroho, kutokana na uongo na uzushi wao umeingiwa na mashaka kuhusu Islam.

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ<sup>12</sup>

Zingatia kuwa hao ndio watu ambao si tu kwamba wamebadili vitabu vya Mungu, bali kwa kuiendeleza dini yao wamelishinda kila taifa katika kuongopa na kwa vile watu hao hawana nuru ile inayoteremka kutoka mbinguni kuusaidia

---

<sup>10</sup> Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

<sup>11</sup> Tunamhimidia Yeye na tunamsalia mjumbe wake mtukufu na Nabii wake muadhamu.

<sup>12</sup> Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na bila shaka kwake tutarejea.

ukweli na inaipambanua kabisa katika dunia dini ya kweli kwa mashuhuda yafululizayo, kwa hiyo watu hao wakalazimika kwa kuwafanya watu waichukie dini iliyo hai, yaani Islam, watumie uzushi wa namna namna na hila na ulaghai na udanganyifu na mambo ya uongo na ya kubuniwa. Ewe mpendwa! Hao ni watu wenye mioyo myeusi ambao hawana hofu ya Mungu na ambao mipango yao ya usiku na mchana ni kujaribu kuwa watu walipende giza na waachane na nuru. Nashangaa sana kwa nini wewe umeathirika na maandishi ya mtu wa aina hii. Watu hao wamewazidi wale wachawi waliozigeuza kamba kuwa nyoka mbele ya Nabii Musa a.s. Lakini kwa vile Musa alikuwa Nabii wa Mungu, basi fimbo yake ikawameza nyoka hao wote. Vivyo hivyo Kurani Tukufu ni fimbo ya Mwenyezi Mungu, kila siku huendelea kuwameza nyoka wa kamba na siku inawadia bali iko karibu ambapo haitabaki hata alama ya nyoka hao wa kamba. Mwandishi wa “Yanaabiul Islam” kama amejaribu kuonesha kuwa Kurani Tukufu imetengenezwa kutokana na visa fulani fulani au kutokana na vitabu fulani, juhudi yake hiyo haifikii hata sehemu ya elfu moja ya juhudi aliyotia mtaalamu mmoja Myahudi kutafuta

chanzo cha Injili. Mtaalamu huyo anafikiri amekwisha thibitisha jambo hili kuwa mafundisho ya Injili kuhusu hulka yamechukuliwa kutoka katika kitabu cha Mayahudi cha Talmud na baadhi ya vitabu vingine vichache vya wana wa Israeli. Na wizi huu umefanyika wazi wazi kabisa kiasi hiki kwamba vifungu kwa vifungu vimenukuliwa neno kwa neno. Mwanachuoni huyo amehakikisha kuwa kweli Injili ni mkusanyiko wa mali iliyoibwa. Kweli amefikia kikomo na hususan yale mafundisho ya mlimani ambayo Wakristo wanajivunia, amehakikisha neno kwa neno kwamba hayo yote ni maneno na vifungu vya Talmud. Vivyo hivyo kwa kunakili ibara zilizoibiwa kutoka ndani ya vitabu vingine amewashangaza watu; matokeo yake, hata watafiti wa Ulaya pia wameelekea upande huu kwa kuvutika sana. Na siku hizi nimesoma jarida moja la Mhindu mmoja aliyejaribu kuthibitisha kwamba Injili ni wizi wa mafundiho ya Budha na kwa kutoa mafundisho ya Budha kuhusu hulka akataka kuhakikisha habari hiyo. Na la kushangaza zaidi ni hili kuwa baina ya wafuasi wa Budha kimeenea kile kisa cha shetani kwamba shetani alimpeleka huko na huko kwa kumjaribu. Hivyo, kila mmoja

ana haki ya kufikiria moyoni kuwa kisa hicho hicho kwa kugeuzwa kidogo kimeingizwa kama wizi ndani ya Injili pia. Jambo hili limethibitika pia kuwa Bwana Yesu lazima alikuja India na kaburi lake liko Srinagar, Kashmir, ambalo tumelithibitisha kwa hoja. Katika hali hii wapinzani wanakuwa na haki zaidi ya kudhania kuwa Injili za sasa kwa hakika ni taswira ya dini ya Kibudha. Mashuhuda hayo mengi yamekwisha tolewa ambayo hayawezi sasa kufichwa. Jambo jingine la kushangaza ni kuwa kitabu cha zamani cha Yuz Asaf ambacho kuhusu hicho watafiti wengi wa Kiingereza nao wanayo maoni kuwa hicho kilienezwa hata kabla ya kuzaliwa Yesu ambacho kimeisha fasiriwa katika nchi zote za Ulaya, Injili inafanana sana na hicho hata kwamba ibara nyingi zinalingana na baadhi ya mifano iliyomo ndani ya Injili, mifano iyo hiyo, kwa maneno yayo hayo, imo pia ndani ya kitabu hicho. Hata mtu awe mjinga sana kana kwamba yu kipofu, yeye naye akikiona kitabu hicho atakuwa na yakini kuwa Injili imekiibia hicho. Ni maoni ya baadhi ya watu kuwa kitabu hicho ni cha Gotama Budha, na kilikuwa awali katika Kisanskrit, kisha kikatafsiriwa katika lugha nyinginezo. Basi,



baadhi ya watafiti wa Kiingereza nao wanaamini hivyo. Lakini kwa kuamini hivyo, Injili inakuwa si chochote wala lolote, na Mungu Apishe mbali, Yesu anathibitika kuwa ni mwizi aliyeiba mafundisho yake hayo. Kitabu kipo, anayetaka akione. Lakini rai yetu ndiyo kuwa hicho ndicho Injili ya Yesu mwenyewe Iliyoandikwa katika safari yake ya India, nasi tumeshathibitisha kwa hoja nyingi kuwa kwa hakika hii ni Injili ya Yesu nayo ni takatifu na safi zaidi kuliko Injili zingine. Lakini baadhi ya wale watafiti wa Kiingereza wanaokichukulia kitabu hicho kuwa ni kitabu cha Budha, wanajichimba wenyewe, na wanamfanya Yesu kuwa mwizi.

Sasa ikumbukwe hii pia kuwa lundo la vitabu vya kidini vya Mapadri ni lundo bovu ambalo ni la aibu kabisa. Watu hao kwa dhana zao tu wanavichukulia baadhi ya vitabu kuwa ni vya kimbingu na vingine vya kubuniwa. Kwao Injili hizi nne ni za asili na zinazobaki takriban hamsini na sita ni za kubuniwa, lakini kwa dhana na shaka tu, siyo kwa dalili yoyote madhubuti. Kwa dhana na shaka tu, siyo kwa dalili yoyote madhubuti. Kwa kuwa kuna mgongano mkubwa baina ya Injili zinazotumika siku hizi na Injili zingine,

hivyo wakaamulia shauri hilo. Lakini maoni ya wahakiki ni kuwa hatuwezi kusema kuwa Injili hizi ni za kubuniwa ama zile ndizo za kubuniwa. Ndiyo maana katika sherehe ya kutawazwa kwa Mfalme Edward Kaisari, mapadri wa London wakavichukua vitabu vyote wanavyovifikiria kuwa vya kubuni, wakavijalidi pamoja na Injili hizo nne katika jalada moja na kumkabidhi mfalme kama zawadi za pongezi. Nakala moja ya jalada hilo ipo kwangu pia. Basi, ni jambo la kutafakari kwamba kama kweli vitabu hivyo vingekuwa vichafu, vya kubuni na visivyo vitakatifu, hapo kuvijalidi vilivyotakasika na visivyotakasika katika jalada moja bila shaka kulikuwa ni jambo la kufanya dhambi sana. Bali, ukweli ni huu kuwa hao watu hawawezi kusema kwa utulivu wa moyo kuhusu kitabu chochote kuwa ni cha kubuni wala cha kweli. Kila mmoja ana njia yake. Na kwa sababu ya chuki sana, Injili zote zinazoafikiana na Kurani Tukufu wanazichukulia watu hao kuwa ni za kubuniwa. Basi, Injili ya Barnaba ambamo kuna bishara kumhusu Nabii wa zama za mwisho s.a.w. imechukuliwa kuwa ni ya kubuniwa kwa sababu tu ndani yake mna bishara wazi wazi kumhusu

Mtume s.a.w. Bwana Sale ameeleza katika maelezo yake ya Kurani Tukufu habari hii pia kuwa ruhubani mmoja wa Kikristo akasilimu baada ya kusoma Injili hiyo. Ilmuradi jambo hili linatakiwa likumbukwe sana kwamba watu hao wasemapo kuhusu kitabu fuani kuwa ni cha kubuniwa au ni uzushi, huwa na sababu mbili tu: 1. Kwanza ni kuwa habari hiyo au kitabu hicho kinahitilafiana na Injii zinazotumika. 2. Ya pili ni hii kuwa habari hiyo au kitabu hicho kinaafikiana na Kurani Tukufu kiasi fulani, na baadhi ya watu washari na wenye nyoyo nyeusi wanajitahidi kwamba kwanza wanataka kueleza kama jambo la kukubalika<sup>13</sup> kuwa vitabu hivi ni vya kubuniwa na kisha husema kuwa visa vyao vimeandikwa ndani ya Kurani Tukufu, na kwa njia hii huwafanya watu wa kawaida wadanganyike. Uhakika wenyewe ni kuwa kuthibitisha maandiko ya zama zile kuwa ya uzushi au ya kweli haikuwa kazi ya yeyote minghairi ya wahyi kutoka kwa Mungu. Basi, wahyi wa Mungu unapolingana na habari fulani, habari hiyo huwa ya kweli ingawa baadhi

---

<sup>13</sup> Ndani ya dini ya Kikristo kuzua na kuongopa kwa kila namna kunajuzu ili kuihami dini, bali ni njia ya kupata thawabu; iangalieni kauli ya Paulo. Mwandishi.

ya majahili wanaichukulia kama kisa tu cha uwongo; na tukio lile ambalo wahyi wa Mungu umelikadhibisha ni la uwongo ingawa baadhi ya watu majahili wanalikubalia kuwa la kweli. Na kuidhania Kurani Tukufu kwamba imetungwa kutokana na visa maarufu au hadithi za kubuniwa au maandiko ya zamani au Injili, ndiyo ujinga wa aibu sana. Je haiyumkiniki kuwa kitabu cha Mungu kilingane na maelezo fulani ya zamani? Mathalani, Ma-veda ya Wahindu yaliyofichikana katika zama zile, kweli zake kadhaa zinapatikana katika Kurani Tukufu. Basi, je, tunaweza kusema kuwa Mtume s.a.w. alikuwa amesoma Ma-Veda pia? Mkusanyiko wa Injili na vinginevyo uliopatikana sasa kwa sababu ya mitambo ya uchapishaji, hakuna katu aliyeujua Uarabuni. Na Waarabu walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Na katika nchi hiyo hata kama alipatikana kwa nadra Mkristo yeyote, huyo naye hakuwa na ujuzi sana wa dini yake<sup>14</sup>. Basi tuhuma hii kuwa Mtume s.a.w. aliviibia vitabu hivyo yaliyomo humo ni

---

<sup>14</sup> Bwana Padri Pfandar amekubali katika kitabu chake *Mizanul Haq* kuwa Wakristo wa Uarabuni pia walikuwa kama watu wasiostaarabika wala hawakuwa na ujuzi. Mwandishi.

fikara ya kulaaniwa. Mtume s.a.w. hakujua kabisa kusoma wala kuandika, hakuweza kusoma hata Kiarabu, sembuse Kiyunani au Kiebrania. Ni jukumu la wapinzani wetu kuhakikisha jambo hili kwamba wataje kitabu chochote cha zamani cha zama zile ambamo kutoka humo yakachukuliwa yaliyomo humo. Na kama yangelikuwa ndani ya Kurani Tukufu mambo fulani yaliyoingizwa humo kwa njia ya wizi, Wakristo wa Bara Arabu waliokuwa adui wakali wa Uislamu mara moja wangelipiga kelele kuwa hayo yameandikwa baada ya kusikia kutoka kwetu.

Ikumbukwe kuwa humu duniani Kurani Tukufu ndiyo kitabu cha pekee<sup>15</sup> kilichodai kuwa ni mwujiza, na ikadaiwa kwa kukazania sana kuwa

---

<sup>15</sup> Kurani Tukufu imejivua kwa kudai kuwa hiyo ni mwujiza na haina kifani chake na imesema kwa kupaza sauti kwamba kama kuna yeyote anayeifikiria kuwa maneno ya binadamu, atoe jibu. Lakini wapinzani wote wakakaa kimya. Ama Injili, basi hiyo Mayahudi walisema katika zama hizo hizo kuwa ni kitu cha wizi. Na Injili haikudai kuwa mwanadamu hana uwezo wa kutunga Injili ya aina hii. Hivyo, Injili yaweza kutiliwa shaka kwamba ni kitu cha wizi siyo Kurani Tukufu; kwani, Kurani Tukufu ndiyo imedai kuwa binadamu hana uwezo wa kutunga Kurani kama hii, na wapinzani wote wakinyamaza wakathibitisha ukweli wa dai hili. Mwandishi.

habari zake na visa vyake vyote vyaeleza habari za ghaibu, na habari za baadaye pia mpaka siku ya kيامa zimo ndani yake. Tena ni mwujiza kwa sababu ya ufasaha wake pia. Basi, ilikuwa rahisi sana wakati huo kwa Wakristo kutolea hadharani baadhi ya visa kuwa hivyo Kurani Tukufu imeviibia kutoka katika vitabu hivyo. Hapo shughuli zote za Islam zingefifia, lakini sasa ndiyo kuomboleza tu baada ya kufiwa. Akili haiwezi kukubali kamwe kuwa Wakristo wa Bara Arabu, kama kweli wangelikuwa na vitabu ambavyo ingeweza kudhaniwa kuwa Kurani Tukufu imechukua visa kutoka ndani ya vitabu hivyo bila kujali vitabu hivyo vilikuwa vya asili au vya kubuniwa, wangenyamaza pasipo kufichua siri. Hivyo, hamna shaka kwamba yote yaliyomo ndani ya Kurani Tukufu yanatokana na wahyi wa Mungu. Na wahyi huo ulikuwa mwujiza wa shani kubwa hata kwamba hakuna mtu aliyeweza kuleta mfno wake. Na ni jambo la kufikiria kuwa mtu aliyeviibia vitabu vingine na akajitungia madhumuni yake mwenyewe huku akijua kuwa madhumuni haya nimechukuwa kutoka ndani ya kitabu fulani na sio mambo ya ghaibu, anawezaje kujasiri kuwaita watu wa dunia nzima kushindana

naye, tena asitokee hata mtu mmoja, wala asiweza yeyote kufichua siri zake. Ukweli ni huu kuwa Wakristo wana hasira sana juu ya Kurani Tukufu, na sababu yenyewe ya hasira ndiyo kuwa Kurani Tukufu imezivunjilia mbali nguvu zote za dini ya Kikristo na imebatilisha kabisa imani ya mtu kuwa Mungu. Imeivunja tikitiki itikadi ya msalaba, na imethibitisha upungufu na ubovu kabisa wa mafundisho ya Injili waliyokuwa wanajivunia Wakristo. Basi, hapo Wakristo lazima wangukuwa na hamaki kwa sababu ya ubinafsi. Hivyo, kiasi chochote watakachozua ni kidogo. Mtu akiwa Mwislamu akitaka kutanasari, mfano wake ni sawa na mtu ambaye baada ya kuzaliwa kutoka tumboni mwa mama yake na kukua, kisha atake kurudi tena tumboni mwa mama yake awe tone la shahawa tena kama alivyokuwa hapo awali. Mimi nastajabu sana kuwa Wakristo wanajivunia nini. Kama wana Mungu, basi ndiye Yule aliyekufa zamani na kaburi lake liko katika Srinagar mtaa wa Khaniyar, Kashmir. Na kama kuna mijuiza yake, basi hiyo si zaidi ya miujiza ya manabii wengine, bali miujiza ya Nabii Eliya imezidi sana kuliko yake. Na kwa mujibu wa kauli ya Mayahudi, yeye hakuonyesha mwujiza wowote,

bali ilikuwa ni ujanja na hila tu.<sup>16</sup> Ama bishara zake, basi nyingi sana hazikutimia. Je, sawa na ahadi wafuasi wake kumi na wawili walijaliwa kupata viti kumi na viwili vya enzi huko peponi? Padri yeyote ajibu basi! Je, Bwana Yesu aliupata ufalme wa kidunia sawa na bishara yake mwenyewe ambao kwa ajili yake hata silaha pia zikanunuliwa? Anene yeyote! Na, je, kwa muafaka wa madai yake Bwana Yesu akashuka katika zama hizo hizo kutoka mbinguni? Mimi nasema achilia mbali kushuka, yeye hata hakujaaliwa kwenda mbinguni. Hayo ndiyo maoni ya wataalamu watafiti wa Ulaya pia. Bali yeye alisalimika kutoka msalabani akiwa nusu mfu, kisha kwa kujificha ficha akatoroka kupitia bara Hindi akafika Kashmir na akafia huko.<sup>17</sup>

---

<sup>16</sup> Kauli hii ya Mayahudi inaungwa mkono na kauli ya Bwana Yesu mwenyewe, kwani Bwana Yesu mwenyewe anasema ndani ya Injili kuwa: “Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara” (Mathayo 12:39). Hivyo, ni dhahiri kuwa kama Bwana Yesu angekuwa amewaonyesha Mayahudi miujiza yoyote, bila shaka angewatajia hiyo wakati Mayahudi walipoomba miujiza. Mwandishi.

<sup>17</sup> Wale watu ambao baada ya kuitwa Waislam wanamfikisha Bwana Yesu mbinguni pamoja na mwili wake, wanatamka neno la upuuzi kinyume cha Kurani Tukufu. Kurani Tukufu ndani ya aya \* **فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي** inadhiihisha kifo cha Bwana Yesu, na



## Chemchem ya Ukristo

---

Kisha hali ya mafaundisho ndiyo kuwa licha ya kutuhumiwa kuwa ya wizi, Injili inakazania tawi moja tu la kuvumilia na kusamehe katika matawi yote ya nguvu ya kibinadamu na kuyaangamiza matawi mengine yote, ilhali kila mtu anaweza kuelewa kuwa chochote mtu alichopewa na kudura ya Muweza hakuna miongoni mwake kitu chochote kisichofaa, na kila nguvu ya mtu imeumbwa kwa masilahi maalum. Na kama vile uvumilivu na msamaha huhesabiwa wakati fulani na mahali fulani kuwa miongoni mwa hulka njema, vivyo hivyo wakati fulani ghera, na kisasi

---

katika aya: # **قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيَ هَلْ كُنْتُ إِلَّا بَشَرًا مِّثْلَ سُوْرًا** yakanusha mtu kwenda mbinguni na kiwiliwili chake. Sasa huu ni ujahili kiasi gani kuwa wanayo itikadi dhidi ya neno la Mungu. Kutoa tafsiri ya *Tawaffa* kuwa kuinulia mbinguni pamoja na mwili ndiyo ujahili ambao hakutakuwa na ujahili wowote mkubwa kuliko huu. Kwanza, katika kamusi yoyote haikuandikwa maana ya *Tawaffa* kuwa kunyanyuliwa mbinguni pamoja na mwili, tena zaidi ya hayo aya **فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي** inapohusiana na kiama, yaani siku ya kiama, Hadhrat Isa a.s. atamjibu Mwenyezi Mungu hivyo, basi inalazimu kuwa kiama kitakuja lakini Bwana Yesu hatakufa na kabla ya kufa atahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu na mwili wake. Kuigeuza Kurani Tukufu hivyo ni kuwapita hata Mayahudi. Mwandishi.

\* Al-Maaida 5:118

# Bani Israaiil 17:94

na kumwadhibu mhalifu huhesabiwa kuwa miongoni mwa hulka bora. Kusamehe na kuachilia mbali kila mara hakufai wala kuadhibu na kulipiza kisasi hakuna hekima. Hayo ndiyo mafundisho ya Kurani, kama Mwenyezi Mungu Anavyosema:

جَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ<sup>18</sup>

Yaani, kadri ya adhabu ya ubaya ni sawa na kadri ya ubaya uliofanywa, lakini yule anayesamehe na katika msamaha huo lengo liwe kurekebisha,<sup>19</sup> basi malipo yake yako kwa Mungu. Hayo ndiyo mafundisho ya Kurani Tukufu. Lakini ndani ya Injili kila mahali imeelekezwa kusamehe tu na kuachilia mbali bila sharti yoyote na kuyaangamiza kabisa masilahi mengine yaliyo msingi wa kuendeshea utamaduni, na imetiliwa mkazo kukuza tawi moja tu miongoni mwa matawi yote ya mti wa nguvu za binadamu na matawi mengine yameachiliwa yasitunzwe. Tena ni ajabu kuwa Bwana Yesu mwenyewe hakutenda sawa na mafundisho ya hulka njema. Alipouona

---

<sup>18</sup> Ash-Shuura, 42:41

<sup>19</sup> Katika Kurani Tukufu haujuzu msamaha usiofaa, kwani kwa njia hii hulka za mtu huharibika na husambaratisha nidhamu yote bali imeruhusu msamaha ule unaoleta marekebisho. Mwandishi.

mtini hauna matunda akaulaani ilhali akawafundisha wengine kuomba dua. Pia akawaamuru wengine kuwa msimwite mwingine mpumbavu, lakini mwenyewe akazidi katika kutoa lugha chafu hata akawaita wazee wa Kiyahudi kuwa ni wana wa haramu. Na katika kila mawaidha yake akawatukana vikali wanazuoni wa Kiyahudi na akawaita majina mabaya. Ni faradhi ya mfundishi wa hulka kwamba kwanza mwenyewe aonyeshe hulka njema. Basi, je, mafundisho mapungufu ambayo hata mwenyewe hakuyatekeleza yanaweza kutoka kwa Mwenyezi Mungu? Mafundisho matakatifu na makamilifu ndiyo ya Kurani Tukufu amabyo yanastawisha kila tawi la mti wa kibinadamu. Na Kurani Tukufu haitilii mkazo upande mmoja tu, bali pengine yafundisha kusamehe na kumwacha mhalifu, sharti kusamehe kunafaa, na wakati mwingine yaagiza kumwadhibu mhalifu kulingana na hali na wakati. Hivyo basi, kwa kweli Kurani Tukufu ni picha ya sheria ya ulimwengu iliyowekwa na Mungu iliyoko daima mbele ya macho yetu. Hili ni jambo linaloingia akilini kuwa maneno na matendo ya Mwenyezi Mungu daima yawiane. Yaani, namna matendo ya Mwenyezi Mungu

yanavyoonekana duniani ndivyo ambavyo ni lazima kitabu cha kweli cha Mwenyezi Mungu kifundishe sawa na matendo Yake; siyo kwamba matendo na maneno yahitilafiane. Tunaona kuwa katika matendo ya Mwenyezi Mungu hakuna kila mara uraufu na msamaha, bali yeye naye anawaadhibu wahalifu kwa adhabu ya namna namna; adhabu za aina hii zimetajwa ndani ya vitabu vya zamni pia. Mungu wetu si Mungu Mpole peke yake bali Yu Mwenye hekima pia, na adhabu zake pia ni kali. Kitabu cha kweli ndicho kinachoafikiana na sheria inayofanya kazi katika ulimwengu, na kauli ya kweli ya Mungu ndiyo isiyohitilafiana na kitendo Chake. Sisi hatujawahi kushuhudia kuwa Mungu anawatendea viumbe wake sikuzote kwa upole na huruma na kwamba haikutokea adhabu yoyote. Hata hivi sasa pia kwa ajili ya watu wenye tabia isiyotakasika Mwenyezi Mungu kwa njia yangu Ametoa habari ya kutokea kwa tetemeko kubwa na la kutisha litakalowaangamiza. Na tauni nayo hajawa na muda mrefu. Ilikuwaje hali ya kaumu ya Nuhu hapo kabla! Kaumu ya Luti ilifikiwa na nini? Hivyo basi eleweni kwa yakini kabisa kwamba kiini cha sheria ni: **تَخَلَّقُوا بِأَخْلَاقِ اللَّهِ** Yaani, kujipatia

hulka ya Mungu Mwenye shani na jalali. Huu ndio ukamilifu wa nafsi. Tukitaka tuwe na hulka njema zaidi kuliko Mungu, basi huku ni kukosa imani na ni utovu wa adabu wa hali ya juu, na pia ni kuzitolea makosa hulka za Mungu.

Hebu fikirieni jambo moja lingine pia, kuwa ni kanuni ya Mungu tangu kale kuwa Yeye husamehe madhambi kwa kutubu na kuomba msamaha, na kwa maombezi ya watu wema Yeye hupokea maombi pia. Lakini kamwe hatujaona ndani ya kanuni ya Mungu Aliyoiweka duniani kuwa Zaidi ajipige jiwe kichwani ndipo Bakari aondokane na maumivu yake ya kichwa. Tena hatujui kuwa watu wengine kuondolewa maradhi yao ya ndani kwa sababu ya Bwana Yesu kujiua ni kwa msingi wa kanuni gani. Na ni falsafa ipi inayoweza kutujulisha kuwa damu ya Bwana Yesu inaweza kuondoa uchafu wa ndani wa mtu mwingine. Bali uchunguzi unatoa ushahidi kinyume chake. Kwani kabla Bwana Yesu alikuwa hajanuia kujiua, Wakristo walikuwa wenye mwenendo mzuri na wenye kumwabudu Mungu. Lakini baada ya tukio la Msalaba, ikawa kama ukingo wa mto kubomoka na maji ya mto kuenea pande zote. Hivyo ndivyo ikawa hali ya

tamaa za nafsi za Wakristo. Hakuna shaka kuwa kama kujiua huku kwa Bwana Yesu kulitokea kwa kunuia kwake, basi akafanya kitendo kisichofaa kabisa. Kama maisha hayo angeyatumia kutoa mawaidha na nasaha, viumbe wa Mungu wangefaidika. Lakini kwa kiendo hicho kisichofaa, watu wengine wamefaidika nini? Naam, kama Bwana Yesu baada ya kujiua angefufuka na mbele ya Mayahudi angepaa mbinguni, Mayahudi wangemwamini; lakini sasa Mayahudi na watu wote wenye akili wanaelewa kuwa Bwana Yesu kupaa mbinguni ni kisa tu na maneno ya porojo.

Isitoshe, itikadi ya Utatu ni itikadi ya ajabu. Je yupo mtu aliyesikia kuwa wawe watatu pia kwa uthabiti na ukamilifu na wawe mmoja pia papo hapo? Na mmoja pia awe Mungu kamili na watatu pia wawe Mungu kamili! Dini ya Kikristo ni dini ya ajabu tu, kuna kosa katika kila jambo na kupotoka katika kila shauri. Tena juu ya magiza hayo yote, wahyi na ufunuo umekoma. Sasa kutoa uamuzi kuhusu makosa ya Injili hizo zote sawa na itikadi za Wakristo haiyumkiniki kwa ufunuo mpya, kwani kwa mujibu wa itikadi zao ufuno hauendelei tena bali umekoma. Sasa mategemeo

yote ni juu ya rai ya kila mmoja ambayo haiepukani na ujinga na giza. Na Injili zao ni mkusanyiko wa mambo ya kipuuzi ambayo ni vigumu sana kuyahesabu; kwa mfano, kumfanya mtu mnyonge kuwa Mungu, na kupendekeza msalaba kwa ajili yake ili kuondoa dhambi za watu na kumpeleka Motoni kukaa humo hadi siku tatu. Na kisha upande mmoja kumfanya Mungu na upande wa pili kunasibisha kwake udhaifu na mazoea ya kuongopa. Ndani ya Injili yamo maneno mengi ambayo, Mungu Apishe mbali, yanathibitisha Bwana Yesu kuwa msema uwongo. Kwa mfano, alimwahidi mwizi mmoja kuwa utafuturu pamoja nami leo huko peponi, lakini kinyume cha ahadi alikwenda Motoni siku hiyo hiyo na kukaa siku tatu mumo humo Motoni. Kadhalika, ndani ya Injili imeandikwa pia kuwa shetani alimpeleka Bwana Yesu huko na huko ili kumjaribu. Ni jambo la ajabu kuwa Bwana Yesu akiwa Mungu hakuweza kuepuka kujaribiwa na shetani, na shetani akawa na ujasiri wa kumjaribu Mungu. Falsafa hii ya Injili ni tofauti na dunia nzima. Kama kweli shetani alimjia Bwana Yesu, basi Bwana Yesu alikuwa na fursa nzuri sana ya kuwaonyesha Mayahudi shetani, maana Mayahudi

walikana kabisa unabii wa Bwana Yesu, kwani ndani ya kitabu cha Malaki iliandikwa alama hii ya Maishi wa ukweli kuwa kabla yake Eliya<sup>20</sup> atarudi duniani mara ya pili. Na kwa kuwa Nabii Eliya hakurudi duniani mara ya pili, basi Mayahudi mpaka sasa wanamwita Bwana Yesu kuwa mzushi na laghai. Hii ndiyo hoja ya Mayahudi ambayo Wakristo hawana jibu lake lolote. Na shetani kumjia Yesu ni fikara ya kimajununi kwa Mayahudi. Majununi wengi hupata ndoto za aina hii hii. Haya ni maradhi ya aina ya jinamizi. Mtafiti mmoja Mwingereza ameeleza kuwa maana ya shetani kumjia ni kuwa Bwana Yesu alipata ufunuo wa kishetani mara tatu, lakini Bwana Yesu hakuathirika na ufunuo wa kishetani. Ufunuo mmojawapo wa kishetani

---

<sup>20</sup> Mayahudi wa zama hizo walimsubiri Nabii Eliya kurudi duniani mara ya pili na kuteremka kutoka mbinguni kama vile masheikh wetu wenye akili ya kawaida wanavyomsubiri Bwana Yesu ashuke kutoka mbinguni. Lakini Bwana Yesu ilimbidi atoe maelezo ya bishara hii ya Nabii Malaki, ndiyo maana mpaka sasa Mayahudi hawamwamini Nabii Isa kuwa Nabii mkweli, kwani Nabii Eliya hajashuka kutoka mbinguni. Kutokana na itikadi hii Mayahudi wakainga Motoni. Hivi sasa Waislamu wamenasa katika tumaini hilo lisilofaa. Hiyo ndiyo kabisa hali ya Mayahudi, lakini haidhuru kwani kwa njia hiyo bishara moja ya Mtume s.a.w. imetimia. Mwandishi.



Yesu alitiliwa moyoni mwake na shetani kuwa amwache Mungu akamfuate shetani pekee. Lakini inashangaza kuwa shetani akamtawala mwana wa Mungu na kumwelekezea dunia, ilhali yuaitwa mwana wa Mungu. Kisha kinyume na kuwa Mungu yeye anakufa. Je, Mungu naye huwa anakufa?

Na kama aliyekufa ni mtu, kwa nini yadaiwa kwamba mwana wa Mungu alikufa kwa ajili ya watu? Tena hana habari ya saa ya kيامa ilhali ajiita Mwana wa Mungu, kama vile Bwana Yesu mwenyewe anavyokiri ndani ya Injili kuwa japo yu mwana wa Mungu, hajui kuwa kيامa kitakuja lini. Juu ya kujiita mwana wa Mungu, kukosa elimu ya habari ya kيامa ni jambo la kipuuzi sana; bali kيامa kiko mbali, yeye hakuwa hata na habari kuwa mtini aliouendea haukuwa na matunda yoyote.

Sasa tunarudia jambo la msingi na kueleza kwa muhtasari kuwa wahyi mmoja wa Mwenyezi Mungu kama uje kwa mwafaka wa kisa au kitabu cha zamani au usiwe unaafikiana kikamilifu au tuseme kisa hicho au kitabu hicho machoni mwa watu ni kitabu cha kubuni au kisa cha kubuni, basi kwa sababu hiyo wahyi wa Mwenyezi Mungu

## Chemchem ya Ukristo

---

hauwezi kushambuliwa. Baadhi ya vitabu Wakristo wanavitaja kuwa vya kihistoria au vya wahyi wa kimbingu, hayo yote hayana msingi yasiyo na uthibitisho wowote, wala hakuna kitabu chao chochote kisichokuwa na taka ya shaka na wasiwasi. Na vitabu wanavyovichukulia kuwa vya kubuni au vya bandia, yumkini visiwe vya bandia; na vile wanavyovichukulia kuwa sahihi, yumkini ndivyo vya bandia. Kitabu cha Mwenyezi Mungu hakihitaji kuafikiana au kupingana navyo. Kipimo cha kitabu cha kweli cha Mwenyezi Mungu siyo kuona vitabu hivyo vyapatana nacho au vyapingana. Kusema kwa Wakrsito kuwa kitabu fulani ni cha kubuni si jambo lililothibitika kwa uchunguzi wa kimahakama, wala kusema kitabu fulani ni sahihi hakutegemei uthibitisho wa kisheria. Haya ni makisio na mawazo tu matupu. Hivyo basi, mawazo yao haya yasiyofaa hayawezi kuwa kipimo cha kitabu cha Mungu. Bali kipimo chenyewe ni kuangalia kuwa kitabu hicho kwa kuafikiana na kanuni ya Mungu Aliyoweka duniani,<sup>21</sup> na kwa miujiza imara chahakikisha

---

<sup>21</sup> Duniani kuna Kurani pekee ambayo imedhihirisha dhati na sifa za Mungu kuafikiana na kanuni ile ya asili ya Mungu

## Chemchem ya Ukristo

---

kuwa kimetoka kwa Mwenyezi Mungu au hapana? Miujiza zaidi ya elfu tatu zilidhihirika kwa Sayyidna na Bwana wetu Mtukufu Mtume s.a.w. na bishara ziko nyingi zisizohesabika. Lakini hatuna haja ya kuelezea miujiza hiyo ya zamani, bali mwujiza mkubwa kabisa wa Mtume s.a.w. ndio huu kuwa wahyi wa manabii wote umekatika na miujiza imepotea na nyimati zao zimebaki mikono mitupu, wanavyo visa tu mikononi mwao, lakini wahyi wa Mtume s.a.w. haukukatika wala miujiza haikuishia, bali daima hudhihirika kwa wafuasi waliokamilika wa umati huu. Ndiyo sababu dini ya Kiislamu ni dini hai na Mungu wake ni Mungu Hai. Basi, na katika zama hizi pia kwa kutoa ushahidi huu nipo mimi mtumishi wa Mungu Mwenye heshima, na kwa mkono wangu mpaka sasa maelfu ya ishara za

---

iliyopo duniani kwa kitendo cha Mungu na ambayo imenakshiwa ndani ya asili na dhamiri ya mwanadamu. Mungu wa Wakristo ni mahabusi tu ndani ya karatasi za Injili, na yule asiye fikiwa na Injili hana habari kabisa ya Mungu huyo. Lakini Yule Mungu anayebainishwa na Kurani, hakuna mtu miongoni mwa wenye akili asiye mjua. Hivyo, Mungu wa kweli ndiye Mungu Yule Aliyeelezwa na Kurani Ambaye ushahidi wake unatolewa na asili ya mwanadamu na kanuni ya Mungu iliyopo duniani. Mwandishi.

kuhakikisha ukweli wa Mtume wa Mungu s.a.w. na Kitabu cha Allah zimekwisha dhihirika, na karibu kila siku mimi nabahatika kufanya maongezi matakatifu na Mwenyezi Mungu. Sasa zindukeni na tafakarini mkaone kwamba kwa kuwa duniani kuna maelfu ya dini zinazonasibishwa kwa Mungu, sasa ithibitikeje kuwa kwa kweli hizo zimetoka kwa Mungu. Kwa vyovyote, kwa dini ya kweli lazima pawepo na kipambanuzi. Na dai la hoja za kiakili tu haliwezi kuwa dalili ya kuhakikisha kuwa dini hiyo imetoka kwa Mungu, kwani maneno yenye akili hata mtu pia anaweza kuyaongea; na Yule mungu anayazalika kwa dalili pekee za kibinadamu, huyo siye Mungu, bali Mungu Yule Anayejidhihirisha kwa ishara zenye nguvu. Ie dini inayotoka kwa Mungu ni lazima kwa uthibitisho wake iwe na ishara kutoka kwa Mungu, na iwe na muhuri wa Mungu ndipo ijulikane kuwa imetoka hasa mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Basi, dini hiyo ni Islam. Mungu Yule aliyefichikana kabisa hutambulikana kwa dini hii, na Anawadhihirikia wafuasi wa kweli wa dini ambayo ndiyo dini ya kweli. Mkono wa Mungu huwa juu ya dini ya haki, na kwayo Mungu Hudhihirisha kuwa Mimi

Nipo. Dini ambazo zinavitegemea visa tu ni sawa kabisa na kuabudu masanamu bila tofauti; ndani ya dini hizo hamna roho ya ukweli. Kama Mungu yu hai hata sasa kama Alivyokuwa zamani, na kama hata sasa Anaongea na Anasikia kama hapo zamani, basi haijulikani sababu yoyote kwa nini anyamaze katika zama hizi, kana kwamba Hayupo. Kama Yeye Haongei katika zama hizi, basi kwa yakini Hasikii pia, kana kwamba yeye si chochote. Hivyo basi, dini ya kweli ndiyo ile inayothibitisha yote mawili — kusikia na kuongea kwa Mungu — katika zama hizi pia. Ilmuradi, katika dini ya kweli, Mwenyezi Mungu Huhabarisha Mwenyewe kuhusu Kuwepo Kwake kwa njia ya maongezi Yake. Kumtambua Mungu ni kazi ngumu sana; si kazi ya wataalamu wa falasfa na wenye hekima wa kidunia kwamba wapate kumtafuta Mungu. Maana, kwa kuangalia mbingu na ardhi inathibitika tu kuwa inatakiwa kuwepo kwa msanii wa muundo huu imara na mkamilifu; lakini haithibitiki kuwa kweli huyo msanii yupo pia. Na tofauti iliyopo kati ya 'anatakiwa awepo' na 'yupo' ni wazi. Basi inayotoa habari hasa ya kuwepo kwake ndiyo Kurani Tukufu pekee ambayo haisisitizi tu kumtambua

Mungu, bali na inamdhihirisha pia. Na hakuna kitabu chochote kingine chini ya mbingu cha kutoa habari ya Huyo aliyefichikana.

Nini shabaha ya dini? Ni hii tu kuwa kwa kupata imani kwa yakini juu ya kuwepo kwa Mungu na sifa zake kamili, mtu aokoze katika tamaa za nafsi, na uzalike upendo hasa wa Mwenyezi Mungu, kwani kwa kweli huo ndio Pepo itakayodhihirika huko akhera kwa sura mbali mbali. Na kutokuwa na habari ya Mungu wa kweli, kujiweka mbali naye na kutokumpenda kikweli ndiyo jahanamu kwa hakika itakayodhihirika kule akhera kwa sura za namna namna. Na shabaha hasa katika njia hii ndiyo kupata yakini kamili juu ya kuwepo kwa Mungu na kisha kumpenda kikamilifu. Sasa yapasa kuangalia ni dini ipi na kitabu kipi kinachoweza kuwa njia ya kupata lengo hili.

Injili yaeleza kwa uwazi kuwa mlango wa maongezi na Mungu umefungika, na njia za kupatia yakini zimefungwa, na yaliyofanyika yamekwisha fanyika zamani, baadaye hakuna kitu. Lakini inashangaza kuwa Yule Mungu anayesikia hadi leo katika zama hizi pia, kwa nini ameshindwa kuongea katika zama hizi! Je,

tunaweza kutulia kwa itikadi hii kuwa katika zama fulani hapo kabla alikuwa anasema na kusikia pia, lakini hivi sasa yeye anasikia tu lakini hasemi. Afaaje Mungu wa aina hii ambaye kwa kupita muda mrefu baadhi ya nguvu zake zikawa hazifai kama mtu akizeeka baadhi ya nguvu zake zinakuwa hazifai! Na tena Mungu wa aina hii anafaa nini ambaye asipofungwa kwenye mti na kupigwa mijeledi na kutemewa mate usoni na kutiwa mahabusu siku chache na hatimaye kutundikwa msalabani, hawezi kusamehe dhambi za watu wake. Sisi tunachukia kabisa Mungu wa aina hii ambaye likamshinda taifa dhalili la Mayahudi lililokuwa limeopoteza hata dola lake. Sisi tunamtambua Yule Mungu kuwa Mungu wa kweli ambaye Akimfanya masikini mmoja wa Makka asiye na wasaidizi kuwa Nabii akaionyesha dunia nzima katika zama hizo hizo onyesho la kudura na ushindi wake hata kwamba mfalme wa Iran alipowatuma maaskari wake kuja kumshika Nabii wetu s.a.w., Yule Mungu Mwenye uwezo Akamwambia Mtume wake, Waambie maaskari kuwa leo usiku Mungu Wangu Amekwishamwua mungu wenu. Sasa yapasa kuzingatia kuwa upande mmoja mtu mmoja

anadai Uungu na hatimaye askari mmoja wa serikali ya Kirumi anamshika na kumsukuma gerezani katika muda wa saa moja au masaa mawili, na maombi yake ya usiku kucha pia hayapokelewi, na upande wa pili kuna mtu anayedai utume tu na Mungu Anawahilikisha wafalme anaowakabili. Msemo huu wamfaa sana mtafuta haki: 'Uwe rafiki wa mshindi ili uwe mshindi'. Tuifanyieje ile dini iliyokwisha kufa? Na twawezaje kunufaika na kitabu kilichokufa, na Yule Mungu anaweza kutunufaisha nini aliye Mungu mfu? Mimi ninaapa kwa Yule Dhati ambaye uhai wangu umo Mikononi Mwake kuwa mimi ninabahatika kupata maongezi halisi na Mungu na karibu kila siku ninaongea naye. Na Yule Mungu ambaye Yesu anamwambia, 'Mbona Umeniacha' mimi naona Yeye Hakuniacha. Na kama Yesu hata mimi pia nimepata kushambuliwa sana, lakini kila mara maadui wakapata kushindwa. Wakala njama ili ninyongwe, lakini mimi sikuwambwa msalabani kama Yesu, bali Mungu wangu Alininusuru katika kila balaa na Akadhihirisha miujiza mikubwa mikubwa kwa ajili yangu na akaonyesha mikono yenye nguvu, na kwa ishara maelfu kwa maelfu Akanithibitishia



## Chemchem ya Ukristo

---

kuwa Mungu hasa ndiye Yule Mungu Aliyeteremsha Kurani Tukufu na ndiye Aliyemtuma Mtume Mtukufu s.a.w. Nami katika mambo haya sioni kuwa Yesu amenizidi chochote. Yaani, kama alivyofunuliwa maneno ya Mungu ndivyo nilivyofunuliwa mimi pia. Na kama vile miujiza inavyonasibishwa kwake, kwa yakini kabisa naiona miujiza hiyo imedhihirika kwangu, bali kumzidi yeye. Na heshima yote hii mimi nimepata kwa kumfuata tu Nabii mmjoja ambaye daraja zake dunia haizijui, yaani Sayyidna Hadhrat Muhammad Mustafa, amani na rehema za Allah ziwe juu yake. Hii ni dhuluma ya ajabu kwamba majahili na wasio na elimu wanasema Bwana Yesu yuko hai kule mbinguni ilhali mimi naona alama za uhai zimo katika Mtume Mtukufu s.a.w. Mungu Yule ambaye dunia haimjui, sisi tumemwona Mungu Huyo kwa njia ya Nabii huyu, na ule mlango wa wahyi uliofungwa kwa mataifa mengine tumefunguliwa kwa baraka za Nabii huyu huyu. Na miujiza inayosimuliwa na mataifa mengine kama visa na hadithi tu, tumeishuhudia kwa njia ya Nabii huyu. Na tumelikuta daraja lile la Nabii huyu ambalo hakuna daraja lolote baada yake, lakini nashangaa

dunia haina habari yake. Wananiambia kwa nini nimedai kuwa Masihi Mau'ud? Lakini nasema kweli kabisa kuwa mtu anaweza kumpita pia Bwana Yesu kwa kumfuata kikamilifu Nabii huyu s.a.w. Vipofu wanasema hii ni kufuru. Mimi ninasema nyinyi wenyewe hamkubahatika kuwa na imani, basi mnajuaje kufuru ni kitu gani? Kufuru imo ndani yenu wneyewe. Kama mngejua aya hii:

<sup>22</sup> إِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ۚ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ  
inamaanisha nini, msingetamka kufuru hiyo. Mungu Anawahimizeni kuwa kwa baraka ya kumfuata Mtume huyu kikamilifu mwaweza kujikusanyia ndani yenu sifa kamili mbali mbali za wajumbe wote wa Allah, nanyi mwaona ni kufuru hata kupata sifa za Nabii mmoja.

Ilmuradi, mwalazimika kuzingatia kwamba dini ya kweli iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu inawezaje kutambulikana? Hivyo basi, ikumbukwe kuwa dini ya kweli ni ile ambayo Mungu Anajulikana kwa kuipitia hiyo. Katika dini zingine juhudi tu za watu zinaelezwa, kana kwamba ndiyo hisani ya mtu aliyomfanya Mungu kumtambulisha. Lakini sawa na mafundisho ya

---

<sup>22</sup> Tuongoze njia iliyonyooka, njia ya wale Uliowaneemesha. Al-Faatiha, 1:6-7

Islam mwenyezi Mungu Mwenyewe katika kila zama hujitambulisha kuwepo kwake kwa sauti ya 'ANAL MAJUUD'<sup>23</sup>, kama alivyojidhihirisha kwangu pia katika zama hizi. Basi, maelfu kwa maelfu ya salaam na baraka zimfikie Mjumbe huyu wa Allah ambaye kwa njia yake tumemtambua Mungu.

Mwishoni, kwa masikitiko makubwa naandika mara ya pili kuwa kauli yako hii kwamba unaona vibaya kumchukua Bi Mariamu kuwa dadake Haruni yaonyesha machoni mwangu kuwa huna elimu sana. Wanazuoni wengi wa zamani pia wameandika mengi kuhusu shutuma hii ya kipuuzi. Kama kwa njia ya istiaru au kwa sababu nyingine Mwenyezi Mungu Alimtaja Mariamu kuwa dada yake Haruni, kwa nini ulishangaa ilhali Kurani Tukufu yenyewe imekwishaeleza mara nyingi kuwa Haruni alikuwepo katika zama za Musa a.s. na kwamba Mariamu huyu alikuwa ni mamake Bwana Yesu aliyezaliwa miaka 1400 baada ya Haruni a.s. Je, hiyo inathibitisha kuwa Mwenyezi Mungu hana habari ya matukio haya, na Akakosea — Mungu Apishe mbali — kumwaita Mariamu kuwa dadake Harun? Ni

---

<sup>23</sup> Yaani 'Mimi Nipo'

wenye hulka mbaya sana watu hao kwani wanafurahi kwa kuleta shutuma mbovu. Na yumkini Mariamu alikuwa na nduguye aitwaye Haruni. Usipokijua kitu, siyo lazima hicho hakipo. Lakini hao watu hawajiangalii wala hawaoni kuwa Injili inapigwa sana kiasi gani. Hebu angalieni, hii ndiyo shutuma kubwa namna gani kwamba Mariamu alitolewa wakfu kwa hekalu ili aitumikie Nyumba Takatifu kwa kudumu, na asiolewe maishani, lakini mimba ya miezi sita, saba ilipobainika wazi ndipo wazee wa kaumu hiyo wakamwozeshwa Mariamu kwa seremala mmoja aitwaye Yusufu. Na kwa kuingia nyumbani mwake Mariamu akajifungua mtoto wa kiume baada ya mwezi mmoja au miwili hivi, akapewa jina Isa au Yesu. Sasa shutuma ndiyo hii kuwa kama kweli mimba hiyo ilikuwa kama mwujiza, kwa nini haikufanywa subira hadi ajifungue? Shutuma ya pili ni hii kuwa ahadi ilikuwa kwamba Mariamu atalitumikia hekalu maisha yote, kwa nini ahadi kavunjwa, akaondolewa katika utumishi wa Nyumba Takatifu, akafanywa kuwa mke wa Yusufu seremala? Shutuma ya tatu ni kuwa kwa mujibu wa Torati ilikuwa haramu na haikujuzu kwa mwanamke kuozechwa akiwa

mjamzito, kwa nini Mariamu aliozeshwa akiwa mjamzito kinyume cha maagizo ya Torati ilhali Yusufu seremala aliichukia ndoa hii, alikuwa na mkewe wa kwanza. Wale watu wanaokataa mitara pengine hawana habari ya ndoa hii ya Yusufu. Ilmuradi, mpinzani ana haki ya kudhani kwamba sababu ya ndoa hiyo ilikuwa kwamba wazee wa kaumu walishuku mimba ya Mariamu kuwa siyo ya halali, ingawa kwa mujibu wa mafundisho ya Kurani Tukufu sisi tunaitakidi kuwa mimba hiyo ilitokana tu na uwezo wa Mungu ili Mwenyezi Mungu Awape Mayahudi alama ya kياما. Na kama ambavyo katika masika maelfu ya wadudu wanazalika wenyewe, na Hadhrat Adam a.s. pia alizaliwa bila baba na mama, basi kwa kuzaliwa huku kwa Yesu hauthibitiki utukufu wake wowote, bali kuzaliwa bila baba ni dalili ya kukosa baadhi ya nguvu. Kwa kifupi, Bi Mariamu akaozeshwa kwa sababu ya shaka tu; waila mwanamke aliyetolewa wakfu kuitumikia nyumba takatifu alikuwa na haja gani ya kuolewa? Ni masikitiko kuwa kwa ndoa hii fitina nyingi zilizalika na Mayahudi waovu wakaeneza shaka za uhusiano usio halali. Basi kama kuna upinzani unaotakiwa kuondolewa ndio huu. Lakini Haruni

kumwita nduguye Mariamu si jambo la kupingwa. Ndani ya Kurani Tukufu halimo neno kwamba Mariamu alikuwa dadake Nabii Haruni; kuna jina tu la Haruni, hamna neno la 'Nabii' humo. Hakika yenyewe ni kwamba Mayahudi walikuwa na desturi ya kuwapa watoto wao majina ya manabii kwa kupata baraka, basi, huenda Mariamu alikuwa na ndugu aliyeitwa Haruni. Kupinga kauli hii ni upumbavu moja kwa moja.

Na kisa cha watu wa pango na vinginevyo kama vimo katika vitabu vya zamani vya Mayahudi na Wakristo pia, na hata kama tufikirie kuwa watu hao wanavichukulia visa hivyo kuwa vya kubuniwa tu, basi haidhuru. Hebu kumbuka kuwa vitabu vyao vya kidini na kihistoria na vitabu vyao vya kimbingu vyote viko gizani. Hujui huko Ulaya siku hizi watu wanavilalamikia kiasi gani, na watu wenye tabia nzuri wenyewe wanaelekea kwenye Islam, na vitabu vikubwa vikubwa vyaandikwa kuitetea Islam, hivyo watu kadha wa nchi za Amerika na nyinginezo wamejiunga ndani ya Jumuiya yetu. Uongo utadumu mpaka lini? Tena ni jambo la kufikiria kuwa wahyi wa Mungu ulikuwa na haja gani ya kuchukua ibara ya vitabu hivyo. Kumbukeni sana kuwa watu hao ni vipofu

na vitabu vyao vyote ni vipofu. Nashangaa, kwa kuwa Kurani Tukufu ilishuka katika kisiwa ambacho wakazi wake kwa kawaida hawakuwa na habari ya vitabu vya Wakristo na Mayahudi, na Mtume Mtukufu s.a.w. mwenyewe hakujua kusoma na kuandika, basi kumtupia Mtume s.a.w. shutuma hizo ni kazi ya watu ambao hawana hofu kabisa ya Mungu. Kama Mtume Mtukufu s.a.w. anaweza kushutumiwa hivyo, basi Yesu atashutumiwa kiasi gani ambaye alijifunza Torati neno kwa neno kwa mtaalamu mmoja Mwisraeli, na alikuwa ametalii vitabu vyote vya Mayahudi, Talmud na kadhalika, na ambaye Injili yake kwa kweli imejaa ibara za Biblia na Talmud sana, nasi kwa sababu ya mwongozo wa Kurani Tukufu tu tunamwamini yeye, waila kuhusu Injili zinapatikana shaka nyingi sana. Ni masikikitiko kwamba ndani ya Injili hakuna hata jambo moja ambalo halimo katika vitabu vya zamani neno kwa neno; basi, kama Kurani Tukufu imeyakusanya pamoja kweli mbali mbali za Biblia kuna nini kilicho kinyume cha akili, na kuna ubaya gani uliofanyika!! Je, waona muhali kwamba visa vyote hivi vya Kurani Tukufu vimetokana na wahyi ambapo Mtume s.a.w. kufunuliwa wahyi ni

jambo linalohibitika kwa hoja imara kabisa. Na nuru na Baraka za unabii wake zinaendelea kudhihirika mpaka sasa. Basi kwa nini wasiwasi wa shetani uingizwe moyoni kuwa, Mungu Apishe mbali, visa vilivyomo ndani ya Kurani Tukufu vimenukuliwa kutoka katika kitabu au maandiko ya zamani. Je, una shaka katika kuwepo kwa Mwenyezi Mungu? Au wewe huamini kwamba Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kujua mambo ya ghaibu? Nami nimeishaeleza kwamba fikara ya Wakristo na Mayahudi kukichukulia kitabu fulani kuwa cha asili na fulani cha kubuniwa ndiyo mawazo tu yote yasiyo na msingi wowote. Hakuna yeyote aliyeuchunguza uhakika wa kilicho cha asili, wala hakuna aliyemkamata mzushi. Kuhusu hiyo, ushahidi wa watafiti wa Ulaya tunao. Hii ndiyo kaumu kipofu ambayo haikubakiwa na mwanga wa imani ndani yake. Na tunawasikitikia sana waliosoma sayansi na falsafa na kuipoteza. Upande mmoja wanazikana mbingu na upande mwingine wanamkalisha Yesu mbinguni. Ukweli ni kuwa kama vitabu vya awali vya Mayahudi ni vya kweli, basi unabii wenyewe wa Bwana Yesu hauthibitiki. Mathalani, kwa Masihi Mauud wa kweli — ambaye Yesu alidai



ndiye yeye — ilikuwa lazima sawa na kitabu cha Nabii Malaki kwamba kabla yake angefika Nabii Eliya duniani mara ya pili. Lakini Eliya hajafika mpaka sasa. Kwa kweli Mayahudi wanatoa hoja kubwa ambayo Yesu hajaweza kujibu barabara. Ni hisani ya Kurani Tukufu juu ya Bwana Yesu kuwa ilitangaza unabii wake. Na suala la kafara, Yesu mwenyewe alishalikataa aliposema mfano wangu ni wa nabii Yona aliyekaa hai siku tatu tumboni mwa nyangumi. Sasa kama yesu kweli alifia msalabani, alifananaje na Yona, na Yona akalinganaje naye? Kwa mithali hii inathibitika wazi kuwa Yesu hakufia msalabani, bali alikuwa amezimia kama alivyozimia Yona. Dawa ya 'Marhamu ya Isa' ambayo imeelezwa katika takriban vitabu vyote vya tiba, katika mada yake imeandikwa kuwa dawa hii ilitayarishwa kwa ajili ya Yesu, yaani kwa ajili ya majeraha yake aliyoyapata msalabani. Mwenye masikio na asikiye.



## **HATIMA YA KITABU**

### **Maelezo juu ya wokovu wa kweli**

Ninaonelea vema kuwa mwishoni mwa kitabu hiki yatolewe maelezo machache kuhusu wokovu wa kweli, maana shabaha na makusudio ya wanadini wote kufuata dini fulani ndiyo kupata wokovu. Lakini inasikitisha kuwa watu wengi hawajui maana ya kweli ya wokovu na wameghafilika nayo. Kwa Wakristo, maana ya wokovu ni kuokolewa katika kuadhibiwa kwa sababu ya kutenda dhambi. Lakini kwa hakika maana ya wokovu siyo hii; kwani yumkini mtu asizini, asiibe, asitoe ushahidi wa uongo, asiue wala asitende dhambi yoyote sawa na elimu yake, hata hivyo asijaaliwe hali ya kupata wokovu na aukose. Kwani, kwa hakika wokovu ndio kujipatia hali nzuri ya kudumu ambayo kiu na njaa yake imewekwa ndani tabia ya asili ya mtu, inayopatikana baada ya kujipatia mapenzi ya dhati ya Mwenyezi Mungu, utambuzi wake kamili na ufungamano naye mkamilifu sharti upendo ububujike kwa kasi pande zote mbili. Lakini mara nyingi kutokana na makosa yake mtu hutamani apate hali nzuri hiyo katika vitu ambavyo kwa

sababu ya hivyo hatimaye taabu na huzuni huzidi zaidi. Basi, watu wengi hutafuta hali hiyo nzuri katika maisha ya anasa, na wakishughulikia usiku na mchana ulewi na tamaa za nafsi mwishowe wanapata kuugua maradhi mbalimbali yanayoangamiza, na hatimaye huaga dunia wakiugua kwa kiharusi, kipooza, kutetemeka mwili, kutetemeka kwa baridi hadi kufa, au donda la matumbo, au donda la ini, ama kwa maradhi ya aibu ya kaswende na kisonono. Na kwa sababu nguvu zao zafifia mapema, hivyo hukosa hata kupata umri wa kawaida na mwishowe wanatambua kuwa vitu walivyodhania kuwa vya kuwaletea hali njema ndivyo hivyo kwa kweli vitu vilikuwa sababu ya maangamio yao. Baadhi ya watu huona raha sana katika kujiongezea heshima ya kidunia na umaarufu na kutafuta vyeo na madaraka, na hawatambui shabaha halisi ya maisha yao, na hawa pia mwishoni wanakufa kwa majuto makubwa. Na baadhi yao wanaendelea kukusanya mali ya kidunia kwa kufikiria labda humo watapata hali njema. Lakini hatimaye wakiacha nyuma akiba yao hiyo yote hunywa kikombe cha mauti kwa taabu, shida na uchungu mwingi. Basi, swali la kuzingata kwa mtafuta haki

ni hili tu kuwa hali nzuri isababishayo furaha ya kudumu itapatikanaje? Na kwa hakika alama ya dini ya kweli ndiyo kwamba dini hiyo ifikishe kwenye hali hiyo bora. Basi kwa mwongozo wa Kurani Tukufu tunapata kujua busara hii ya ndani sana kuwa hali hiyo bora ya kudumu imo ndani ya kumtambua vema Mwenyezi Mungu, kisha imo katika mapenzi matakatifu makamilifu ya dhati ya Huyo wa Pekee na katika imani kamili ambayo itie moyoni kiherehere cha kiupendo. Maneno hayo kwa kusema ni machache, lakini kuielezea hali ya kaifa yake daftari kubwa haiwezi ikatosha. Ikumbukwe kuwa kuna alama nyingi za utambuzi sahihi wa Mungu Azizi Mtukufu. Kati ya hizo, mojawapo ni hii pia kuwa kudra yake, Umoja wake, ujuzi wake na kila uzuri na sifa yake isitiliwe doa la nakisi kwani kama Yule Ambaye kila chembe iko chini ya amri yake na ambaye roho zote tele tele na muundo wa mbingu na ardhi uko chini ya utawala wake, Ana kasoro katika kudra zake na hekima zake na nguvu zake, basi kazi za ulimwengu wa kiwiliwili na wa kiroho haziwezi kuendelea katu. Mungu Apishe mbali, kama iaminiwe kuwa chembecheme na nguvu zake zote, na roho na nguvu zao zote zipo tu

zenyewe pasipo kuumbuwa, itabidi kuamini kuwa ujuzi wa Mwenyezi Mungu na Umoja wake na kudra zake, vyote hivyo vitatu, vina kasoro. Kwani, kama roho zote na chembechembe zote hazikuumbwa na mkono wa Mwenyezi Mungu, basi hakuna sababu tuwe na yakini kuwa Mwenyezi Mungu Anajua hali za undani wa vitu hivyo. Na maadamu hakuna dalili ya ujuzi wake — bali dalili iko kinyume chake — basi yalazimika kuwa Mwenyezi Mungu pia hana habari ya asili ya vitu hivyo kama sisi, ujuzi wake hauzizunguki sifa za ndani sana za hivyo zilizofichikana. Ni dhahiri kabisa kwamba kama, kwa mfano, dawa fulani inategenezwa kwa mikono yetu, au mbele ya macho yetu inatayarishwa dawa ya sharubati au majimaji ama vidonge, au maji ya dawa kadha yanatolewa kwa kukeneka, basi kwa vile sisi ndio watengenezaji wa dawa hizo, tunazifahamu dawa hizo zote na tunafahamu vizuri kuwa hizi ni dawa fulani fulani, ina uzito fulani na imetegenezwa kwa madhumuni fulani. Lakini kama kuna maji ya dawa ya kukenekwa ama vidonge au dawa ya majimaji isiyojulikana hakika yake ambayo hatukuitengeneza wala hatuwezi kutenganisha

dawa za mchanganyiko huo, basi lazima hatutakuwa na habari ya dawa hizo. Na ni dhahiri shahiri kuwa kama Mwenyezi Mungu Aaminiwe kuwa Yeye ndiye mwumbaji wa chembechembe na roho zote, basi itatubidi papo hapo kuamini kuwa lazima Mwenyezi Mungu Anayo elimu pia ya nguvu zilizofichikana za chembechembe na roho hizo zote. Na uthibitisho wake ni kuwa Yeye ndiye mwumbaji wa nguvu zote hizo, na mtengenezaji hawezi kukosa kujua kitu alichokitengeneza mwenyewe. Lakini, kama yeye siye mwumbaji wa nguvu hizo, basi hoja yoyote haiwezi kuhakikisha kuwa Yeye anayo elimu ya nguvu zote hizo. Kama msemi bila dalili kuwa yeye Anayo elimu, basi huko ni kutumia tu nguvu, na ni dai tupu. Lakini kama ambavyo tunayo hoja kuwa mtengenezaji lazima huwa na elimu ya kitu alichotengeneza, wewe kinyume chake una hoja gani kuwa vile vitu ambavyo hakuviumba Mwenyezi Mungu mwenyewe, Yeye Anazijua nguvu zake zote zilizofichikana. Maana, vitu hivyo siyo dhati yenyewe ya Mwenyezi Mungu ili kama Anavyojijua avijue pia; bali kwa mujibu wa itikadi ya dini ya Arya vitu vyote vyenyewe ni mungu wao na vyenyewe havina mwanzo, ni vya

kale. Na kwa kuwa havikuumbwa na ni vya kale, hivyo havina uhusiano wowote na Mungu hata kwamba kama idhaniwe kuwa Mungu amekufa, vitu hivi havina shida yoyote, kwani kwa kuwa Mungu siye mwumbaji wa nguvu hizo, basi hata kwa kubaki vitu hivi havimhitaji Mungu kama ambavyo havikumhitaji kwa kuumbika. Na Mwenyezi Mungu Ana majina mawili: moja Hayyi la pili Qayyumu. Hayyi maana yake Aliye Hai Mwenyewe na mwenye kuwapa uhai wengine, na Qayyum maana yake ni Anayejitegemea kuwa Mzima wa milele na mwenye kuvibakiza vitu Alivyovumba. Hivyo basi, kila kitu kinaweza kufaidika kwa jina Qayyumu la Mwenyezi Mungu ambacho kilikwisha faidika hapo awali kwa jina lake Hayyi, kwani Mwenyezi Mungu Huvihifadhi vitu Alivyoviumba, siyo vile vitu ambavyo mkono wa Mwenyezi Mungu haukuvigusa kabisa. Kwa hiyo, Yule mtu anayemwamini Mwenyezi Mungu kuwa Hayyi, yaani Mwumbaji, ndiye mwenye haki ya kumwamini kuwa Qayyumu pia, yaani Mwenye kuvitegemeza kwake Alivyoviumba. Lakini Yule mtu asiyemwamini Mwenyezi Mungu kuwa Hayyi, yaani Mwumbaji, hana haki ya kuitakadi



kwabma yeye anavisaidia ili vibaki. Kwani kuvisaidia kwamaanisha kuwa Asipovisaidia vitatoweka vitu hivyo. Na ni dhahiri kuwa vile visivyotokana kwake, vitu hivyo haviwezi kumhitaji ili kubaki. Na kama vinamhitaji kubaki, basi vinamhitaji hata katika kuzaliwa. Ilmuradi, majina haya mawili, Hayyi na Qayyumu, ya Mwenyezi Mungu yanalingana katika kuathiri, wala hayawezi kamwe kutengana. Hivyo basi, wale watu wanaoamini kuwa Mungu siye mwumbaji wa roho na chembechembe, hao wakitumia akili na fahamu kidogo, watalazimika kukiri kuwa Mungu siye Qayyum pia wa vitu hivyo, yaani hawawezi, kusema kuwa roho au chembechembe zimeumbwa na Mwenyezi Mungu. Bali, vile vitu vinahitaji msaada wa Mwenyezi Mungu vilivyoubwa naye. Kitu kingine kisichomhitaji kwa kuumbika chamhitajije msaada wake ili kubaki? Dai hilo halina dalili yoyote. Nasi tumeshaandika sasa hivi kuwa kama ikubaliwe kuwa roho na chembechembe tangu azali zipo tu zenyewe pasipo kuambwa, hapo hakuna hoja inayoweza kuthibitisha kuwa Mwenyezi Mungu Anazijua sifa zao zinazofichikana. Na nguvu zao zinazofichama. Na

kusema kwamba kwa kuwa huyo ni Mungu wao, basi anajua tu sifa zao na nguvu zao zilizofichikana, hili ni dai tu lisilohakikishwa kwa hoja yoyote wala dalili, wala haikuthibitishwa kuna uhusiano wa utumishi na Uungu baina yao; bali yeye si Mungu wao katu. Yule asiyeziumba chembechembe wala roho anawezaje kuwa Mungu wao? Na kwa maana gani tunaweza kusema kuwa Yu Mungu wa roho na chembechembe, na uhusiano huu unaweza kuwa kwa misingi gani kuwa Mungu ndiye Mungu wa roho na chembechembe? Uhusiano unakuwa ama wa miliki, kwa mfano isemwe kuwa mtumishi wa Zaid — hapa inatakiwa kuwepo sababu ya kumilikiwa, na haijulikani kwa nini vitu vilivyo huru vyenye nguvu zao tangu azali viwe miliki ya Mungu bila sababu yoyote — au uhusiano unakuwa wa nasaba, kama vile isemwe kuwa “mwana wa Zaid”. Lakini kwa kuwa roho na chembechembe hazihusikani na Mungu kwa mahusiano ya utumishi na Mungu, basi uhusiano huu pia haujuzu. Na katika hali hii, ni kweli kabisa kwamba roho zisizohusika na Mungu hazina faida ya kuwepo kwa Mungu wala hazina madhara ya kutokuwepo kwake. Bali, katika hali hii wokovu

ambao Waarya wanaita *Mukti* ni jambo lisilowezekana, tena linakataliwa. Kwani, mategemeo yote ya wokovu ni upendo wa dhati ya Mwenyezi Mungu. Na upendo wa dhati ndio mapenzi yaliyohulukiwa na Mwenyezi Mungu ndani ya asili ya roho. Na ikiwa roho hazikuumbwa na Mungu, zinawezaje kuwa na upendo asilia kwa Mungu? Na lini na waktai gani Mungu aliingiza mkono wake katika tabia yao ya asili, na kutia humo mapenzi haya? Hii haiyumkiniki, kwani mapenzi haya ya asili ndiyo ule upendo ambao uwe umeambatana tangu azali na tabia ya asili, wala usiwe unazalika huko nyuma, kama Mwenyezi Mungu Anavyoashiria ndani ya Kurani Tukufu kwenye hiyo katika kauli yake hii:

أَكْسَتْ بِرَبِّكُمْ قَالُوا بَلَىٰ<sup>24</sup>

Yaani, Mimi niliziuliza roho kuwa je, Mimi si mwumba wenu? Roho zikajibu kuwa naam. Maana ya aya hii ni kwamba ndani ya asili ya roho ya mwanadamu umo ushahidi kuwa Mungu ndiye Mwumba wake. Hivyo, basi, roho ina upendo wa Mwumba wake kitabia na kiasili,

---

<sup>24</sup> Al-A'raaf, 7:173

maana, hiyo ni kiumbe chake, na kwenye hiyo inaashiria aya hii ya pili kama Mwenyezi Mungu Anavyosema:

فَطَرَتِ اللَّهُ التِّي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا<sup>25</sup>

Yaani, hamu ya roho kumtafuta Mungu Mmoja Asiyeye na mshirika na kukosa faraha ya kweli bila kumpata, imo ndani ya asili ya mwanadamu. Yaani, Mungu Amekwishatia hamu hii katika roho ya mwanadamu kuwa roho ya mwanadamu haiwezi kupata utulivu wala raha kutoka kwa kitu chochote isipokuwa kwa kuungana na Mwenyezi Mungu. Hivyo basi, kama hamu hii imo ndani ya roho ya mwanadamu, ni lazima tukubali kuwa roho imeumbwa na Mwenyezi Mungu Ambaye Alitia hamu hii ndani yake. Na ukweli ni huu kwamba hamu hii imo ndani ya roho ya mtu, basi imethibitika kuwa kwa kweli roho ya mtu imeumbwa na Mungu. Ni desturi kuwa kadri unavyokuwa uhusiano baina ya vitu viwili, kadiri hiyo hiyo huzalika upendo baina yao kwa sababu ya uhusiano huo, kama vile mama alivyo na mapenzi kwa mtoto wake, na mtoto kwa mama yake, kwani huyo amezaliwa kwa damu yake na

---

<sup>25</sup> Ar-Ruum, 30:31

amelelewa tumboni mwake. Basi, kama roho hazina mahusiano yoyote na Mwenyezi Mungu ya kuumbwa naye, nazo zipo tu zenyewe tangu azali, hapo akili haiwezi kukubali kuwa ndani ya asii yao hamna mapenzi ya Mungu, basi kwa vyovyote vile roho hizo haziwezi kupata wokovu.

Hakika hasa na chimbuko la kweli la wokovu ni upendo wenyewe unaomfikisha mtu hadi kuungana na Mungu. Sababu yake ni kuwa hakuna mpendaji anayeweza kukaa mbali na mpenzi wake. Na kwa vile Mungu Mwenyewe ni nuru, hivyo kwa kumpenda Yeye nuru ya wokovu huzalika; na ule upendo uliomo ndani ya asili ya mtu unayavuta kwake mapenzi ya Mwenyezi Mungu; kadhlika mapenzi binafsi ya Mwenyezi Mungu hutilia harara isiyo ya kawaida ndani ya mapenzi binafsi ya mwanadamu; na kwa kukutana na mapenzi haya mawili huzalika hali ya mauti na kisha nuru huzalika ya kubakia na Mungu. Na jambo hili kwamba kukutana kwa mapenzi hayo mawili lazima kunaleta matokeo kuwa mwisho wa mtu wa aina hii uwe mauti, na dhati yake (iliyo pazia) ikiwa kama majivu, roho ijipoteze kabisa katika Upendo wa Mungu. Mfano wake ni ile hali ambapo mtu anaangukiwa na radi kutoka

mbinguni, hapo kutokana na mvuto wa moto wake hujitokeza nje papo hapo moto wa ndani ya mwili wa mtu, na matokeo yake huwa mwili kuangamia. Basi, kwa hakika kifo hiki cha kiroho pia kinahitaji moto wa aina mbili, moto mmoja wa mbinguni na mmoja wa ndani. Na kwa kukutana na mioto hii miwili huzalika mauti ambayo pasipo hayo safari ya roho haiwezi kukamilika. Mauti hayo ndiyo kitu ambapo safari ya wamwendeao Mungu humalizika na hapo ndipo mpaka wa mwisho wa juhudi za mwanadamu. Baada ya mauti hayo, mtu hupata daraja ya kubakia ikiwa ni fadhili na upaji, na huko ndiko inakoashiria aya hii:

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ<sup>26</sup>

Kwa kifupi muradi wa aya hii ni kwamba kila aliyepata daraja hii kaipata kama neema. Yaani, kwa fadhili tupu, kama malipo ya kitendo fulani.<sup>27</sup>

---

<sup>26</sup> Al-Faatiha, 1:7

<sup>27</sup> Kwa vile mtu kutokana na udhaifu wake wa kibinadamu hawezi kutenda matendo ya kumfanya astahiki kupata neema nyingi zisizo na mipaka wala mwisho — na bila kuzipata neema hizo hawezi katu kuupata wokovu wa kweli — ndiyo maana mwanadamu anapokwishafanya juhudi na ibada kwa nguvu zake zote na uwezo wake wote, ndipo ukarimu wa Mungu kwa kumhurumia kwa fadhili zake tu humsaidia kwa kuona unyonge wake, na bila malipo yoyote humpatia neema

## Chemchem ya Ukristo

---

Na haya ndiyo matokeo ya mwisho ya mapenzi ya Mungu yanayoleta uzima wa milele na kuokoa katika mauti. Uzima wa milele si haki ya yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mzima wa milele. Hivyo, miongoni mwa wanadamu, yule tu hupata uzima wa milele anayetengana na mapenzi ya wengine na akijipoteza ndani ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake binafsi anapata kutoka kwake sehemu ya maisha ya milele kwa njia ya kivuli. Na haifai kusema kumhusu mtu wa aina hii kuwa yu mfu, kwani amehuika akiwa ndani ya Mungu. Wafu ndio wale waliokufa wakikaa mbali na Mungu. Basi, makafiri na wasio na dini na washirikina ndio wale ambao pasipo kupata mapenzi ya dhati na kutokuungana na Mungu wanaziamini roho kuwa zipo tu zenyewe tangu azali. Bali ukweli ni huu kuwa hakuna uzima bila ya Mungu. Mungu tu ndiye Anayeitwa Mzima. Kisha chini ya kivuli chake na kwa kujipoteza ndani ya mapenzi yake, roho za wanaoungana naye zinapata uhai wa kweli. Na bila ya kuungana naye, uzima hauwezi kupatikana. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu ndani

---

ile ya kukutana na Mungu walyopewa watawa wa kabla yake. Mwandishi.

ya Kurani Tukufu anawaita makafiri kuwa wafu, na Anasema kuwahuu watu wa motoni:

إِنَّهُ مَنْ يَأْتِ رَبَّهُ مُجْرِمًا فَإِنَّ لَهُ جَهَنَّمَ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ<sup>28</sup>

Yaani, mtu atakayekutana na Mola wake akiwa mkosefu, atapata jahannamu. Hatakufa humo wala hatakuwa hai. Yaani, hatakufa kwa sababu yeye ameumbwa kwa kuabudu kudumu, hivyo, kuwepo kwake ni lazima; wala hatuwezi kusema kuwa yu hai, maana uhai wa kweli unapatikana kwa kuungana na Mungu na uhai wa kweli ndio wokovu hasa, nao hauwezi kupatikana bila yakuwa na mapenzi ya Mungu na kuungana na Mungu Mtukufu. Kama watu wengine wangejua hekima ya uhai wa kweli, kamwe wasingedai kuwa roho zote zipo tu zenyewe tangu azali bila kuumbwa na zina sehemu katika uhai wa kweli. Ukweli ni huu kuwa hizi ni elimu za kimbinguni na huteremka tu kutoka mbinguni, na waja wa kimbinguni tu wanajua uhakika wake ambapo dunia haina habari nayo.

Sasa tukirudi kwenye habari yenyewe tunaandika kuwa chemchemi ya wokovu wa milele ni mwungano na Mungu, na yule tu hupata wokovu

---

<sup>28</sup> Twaa Haa, 20:75



## Chemchem ya Ukristo

---

anayekunywa maji ya uhai kutoka katika chemchemi hii. Mwungano huo hauwezi kupatikana pasipokuwa na utambazi kamili, upendo kamili, uaminifu kamili na Imani kamili. Na alama ya kwanza ya utambuzi kamili ni kuwa elimu kamili ya Mwenyezi Mungu isitiliwe doa lolote. Na sasa hivi tumekwisha hititisha kuwa wale watu wanaoamini kuwa roho na chembechembe za miili zipo zenyewe na tangu azali, hao hawamwamini Mwenyezi Mungu kuwa mjuzi wa mambo ya ghaibu kwa ukamilifu. Ndiyo maana wanafalasca wapotofu wa Kiyunani waliofikiria kuwa roho zipo zenyewe na zipo tangu azali walikuwa na itikadi kuwa Mungu hajui maelezo madogo madogo ya mambo. Kwa sababu, katika hali ambapo roho na chembechembe za ulimwengu zipo tangu azali na zipo tu zenyewe, na kuwepo kwa vitu hivi siyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi hakuna hoja yoyote inayoweza kuhakikisha kuwa Mungu Anazijua nguvu zao za ndani kwa ndani na siri zao zilizofichika. Hii ni dhahiri kuwa elimu kamili anayoweza mtu kuwa nayo kuhusu hali za ndani za vitu vilivyotegenezwa kwa mkono wake mwenyewe pamoja na kaifa na maelezo yote,

hiyumkiniki ajue kitimilifu na kikamilifu hali zilizofichika za vitu vingine. Bali ndani ya elimu zingine kuna uwezekano wa kukosea. Hivyo, hapa wale wanaodai kuwa roho na chembechembe zipo tu zenyewe na zipo tangu azali wanalazimika kukiri kwamba elimu ya roho na chembechembe inayolingana na shani ya Mungu — yaani kama vile Mungu ni mkamilifu elimu ile pia iwe kamilifu — mungu wao hanayo kutokana na itikadi hii (ya kuwa roho na chembechembe zipo zenyewe na zipo tangu azali). Na kama mtu aseme kuwa anayo elimu hiyo, basi anawajibika kuthibitisha hiyo kwa dalili iliyo wazi na wala siyo kwa madai tu. Ni dhahiri kuwa katika hali ambapo roho zipo zenyewe tangu azali, na zenyewe ni Mungu wao, basi inamaanisha kana kwamba roho zote zinakaa katika eneo lao la pekee zinalomiliki kwa kudumu na Mungu Anakaa mbali, hakuna mahusiano yoyote kati yao. Tena hawawezi kueleza sababu ya jambo hili kuwa juu ya roho na chembechembe zote kuwepo tangu azali na kuwepo zenyewe tu, kwa nini zimekuwa chini ya mamlaka ya Mungu? Je, hiyo ikatokea baada ya vita au mapigano yoyote ama roho zenyewe kwa kufikiria maslahi fulani

zikasalimu amri. Na kwa mujibu wa itikadi zao ingawa Mungu wao ni Mkarimu na Mwadilifu, lakini hata hivyo hahurumii wala hafanyi uadilifu, kwani kwa kuficha unyonge wake, hazipi roho wokovu wa milele. Sababu yake ni hii kuwa kama akizipa roho wokovu wa milele, hapo yalazimu kuwa wakati fulani roho hizo zikipata wokovu, zisirudi mara kwa mara duniani, ilhali Mungu Anataka dunia iendelee ili utawala wake uendelee kustawi, ndiyo maana yeye hataki katu kuipa roho yoyote wokovu wa milele. Bali, ingawa roho yoyote hata kama ifikie daraja ya Autaar<sup>29</sup>, au Rishi au Siddh, hata hivyo mara kwa mara huziingiza katika mzunguko wa kuja duniani tena na tena. Lakini, je, tunaweza kumnasibisha Mungu Mweza na Mkarimu sifa hizi duni kuwa Akiwaudhi watumishi wake na anafurahia, lakini hataki kuwapa utulivu wa kudumu? Mungu Mtakatifu hawezi kunasibishwa na ubahili kiasi hiki. Inasikitisha kuwa mafundisho ya ubahili wa namna hi yanapatikana pia ndani ya vitabu vya Wakristo. Hao wanaamini kuwa mtu asiyemkubali Yesu kuwa Mungu, huyo ataingia katika

---

<sup>29</sup> Autar, Rishii (Nabii, Mtume)

Siddh, Pandit, Sheikh wa Kibaniani, Mja wa Mungu

Jahanamu ya milele. Lakini Mwenyezi Mungu Hakutufundisha hivi; bali hufundisha kuwa makafiri wakikaa katika jahanamu muda mrefu kisha watapata sehemu ya rehema ya Mwenyezi Mungu kama ilivyo ndani ya Hadithi pia:

يَأْتِي عَلَىٰ جَهَنَّمَ زَمَانٌ لَّيْسَ فِيهَا أَحَدٌ وَ نَسِيمُ الصَّبَا تُحَرِّكُ أَبْوَابَهَا

Yaani, zama zitawadia kwa jahanamu ambapo hamtakuwamo humu yeyote, upepo mwanana wa Mashariki utaitikisa milango yake. Kuafikiana na hiyo kuna aya hii katika Kurani Tukufu:

إِلَّا مَا شَاءَ رَبُّكَ ۗ إِنَّ رَبَّكَ فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيدُ<sup>30</sup>

Yaani, watu wa motoni watakaa katika Jahanamu sikuzote, lakini Mungu Atakapopenda atawaondoa kutoka katika Jahanamu, kwani Mola wako Huweza kufanya Anavyotaka. Mafundisho haya yanaendana na sifa kamilfu za Mwenyezi Mungu, maana, Yeye Ana sifa za kijalali na za kijamali pia, naye ndiye Anayejeruhi na ndiye Anayetia marahamu pia.<sup>31</sup> Jambo hili ni kinyume cha akili

---

<sup>30</sup> Huud, 11:108

<sup>31</sup> Jambo hili lenyewe ni kinyume na akili kuwa mtu apewe adhabu ya milele kama Mungu Alivyo wa milele na hivyo watu wa motoni wadumu milele motoni sawa na umilele wa Mungu. Kwa vyovyote Mungu naye Anahusika na makosa yao kwani Yeye ndiye Aliyeziumba nguvu zilizo dhaifu. Hivyo

na dhidi ya sifa kamilifu za Mungu Mwenye shani kuwa baada ya kuwatia motoni, sifa zake za kuadhibu tu ndiyo zijitokeze sikuzote, lakini sifa ya huruma na msamaha isitaharuki, na sifa za ukarimu na huruma zionekane kama zimeondoshwa. Bali, yaonekana kutokana na Alichosema Mwenyezi Mungu ndani ya Kitabu chake Kitukufu, kwamba watu wa Motoni watakaa kwa muda mrefu ulioitwa 'milele' kiistiara kwa sababu ya udhaifu wa kibinadamu, kisha sifa ya huruma na ukarimu itajitokeza kwa nguvu na Mungu Atatia mkono wake motoni na kadiri watakaolingia katika gao lake, hao wote watatolewa motoni. Hivyo, katika Hadithi hii pia iko ishara kwenye wokovu<sup>32</sup> kwa wote, maana kama alivyo Mungu, gao la Mungu nalo halina mipaka, basi hakuna yeyote anayeweza kubaki nje yake.

---

watu wa Motoni wana haki ya kufaidika na udhaifu huo walioupata ndani ya asili yao kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mwandishi.

<sup>32</sup> Kwa wokovu hailazimiki kuwa watu wote wawe katika daraja moja; bali wale waliojichagulia Mungu hapa duniani, nao wakajipoteza ndani ya mapenzi ya Mungu na wakaimarika katika njia iliyonyooka, hao wanazo daraja maalum, watu wengine hawawezi kufikia daraja hizo. Mwandishi.

Ikumbukwe kuwa kama vile nyota zinavyoendelea kuchomoza sikuzote kwa zamu, ndivyo hivyo sifa za Mwenyezi Mungu pia zinavyoendelea kuchomoza; pengine mwanadamu anakuwa chini ya kivuli cha sifa za Mungu za kijalali, na pengine kivuli cha sifa za Mungu za kijamali humwangukia. Ndiko Mwenyezi Mungu Anakoashiria Anaposema:

كُلُّ يَوْمٍ هُوَ فِي شَأْنٍ<sup>33</sup>

Basi, ni wazo la kijinga kabisa kufikiria kwamba baada ya wahalifu kutiwa motoni sifa za ukarimu na huruma zitatanguka kwa kudumu wala kamwe hazitajitokeza tena, kwani sifa za Mungu haziwezi kuondoshwa. Bali, sifa ya kweli ya Mwenyezi Mungu ni upendo na huruma, na hiyo ndiyo mama wa sifa zote. Na hiyo ndiyo pengine inachemka kwa sura ya sifa za kijalali na kighadhabu ili kumrekebisha mtu, na pindi anaporekebeka upendo hujitokeza kwa sura yake na kisha hudumu kama upaji. Mungu si kama mtu mwenye hamaki amabye awe na shauku ya kutoa adhabu hivi hivi tu. Yeye Hamdhulumu yeyote, bali watu hujidhulumu wenyewe. Wokovu wote umo

---

<sup>33</sup> Yaani, kila siku Yeye Huwa katika shani tofauti. Ar-Rahmaan, 55:30

katika kumpenda, na adhabu yote imo katika kutengana naye.

Hayo ndiyo mafundisho ya wafuasi wa Aray Samaj kuhusu utambuzi wa Mungu. Kwa mafundisho hayo inabidi kuamini kuwa kila mmoja anayepata heshima mbele ya Mweneyzi Mungu, hata kama akawa Autaari au Rishii au yule ambaye anashushiwa Maveda, heshima yake haiwezi kuaminika kamwe, bali mara elfu yeye huondolewa kwenye kiti cha heshima. Japo yeye alikuwa mpendwa sana wa permeshar (Mungu) na alikuwa amemkurubia sana, na alikuwa Autaar, na Rishii na kadhalika, lakini akiingia katika duara la Avagoni<sup>34</sup> hugeuka kuwa mdudu fualni, kamwe wokovu wa milele haupati. Hapo napo hofu ya kufa, kisha baada ya kufa hofu ya adhabu ya *Avagoni!* Ilimuradi, hivyo haki ya Mungu imetolewa. Upande mmoja roho na chembechembe zote katika kuwapo zenyewe tangu azali zimeshirikishwa naye, na upande wa

---

<sup>34</sup> Avagoni katika dini ya Arya inamaanisha kwamba kila mmoja anayekufa huzalika tena duniani kwa sura nyingine kama vile mnyama fulani au mdudu na kadhalika kulingana na vitendo vyake alivyotenda maishani. Kazalika huku mara kwa mara hakuna mwisho wake. Mwenezi.

pili Permeshar (Mungu) ameonyeshwa kuwa bahili kiasi hiki kwamba ingawa ana nguvu na ni mwenye uwezo wote lakini hata hivyo hataki kumpa yeyote wokovu wa kudumu.

Kisha, yale ambayo Veda imewafundisha watu ili wapate kutakasika, uhakika wake unadhihirika vizuri kutokana na mafundisho ya Nyoga ambayo muhtasari wake ni kuwa Mwarya kwa ajili ya kupata kizazi anaweza akamruhusu mke wake wa ndoa kulala na mwanamume yeyote mwingine. Na kabla mwanamke huyu hajapata watoto kumi na mmoja kutokana na tendo hili 'tukufu' anaweza kuendelea kulala na mtu huyo mgeni. Baada ya hayo, sasa tunarejea kwenye shabaha yenyewe, nayo ndiyo kuwa kufuatana na mafundisho ya Maarya, Permeshar (Mungu) wao hawezi kuwa mjuzi wa ghaibu, na hawanayo dalili ya kuonyesha kuwa Permeshar (Mungu) ni mwenye kujua habari za ghaibu.

Vivyo hivyo kutokana na itikadi ya Wakristo, Mwenyezi Mungu si Mjuzi wa mambo ya ghaibu. Kwani Yesu amechukuliwa kuwa Mungu na yeye mwenyewe anakiri kuwa mimi niliye mwana wa Mungu sina elimu ya kiyama, basi matokeo yake



## Chemchem ya Ukristo

---

yanaweza kuwa nini isipokuwa tu kuwa Mungu hajui kiyama kitatokea lini.

Kisha tawi la pili la utambuzi maarifa sahihi ni kutambua uwezo kamili wa Mwenyezi Mungu. Lakini katika tawi hili pia Maarya na Mapadri wanamtia doa Mungu wao.

Maarya wamtia Mungu doa kwa njia hii kuwa wao hawamwamini *Permeshar* (Mungu) wao kwamba anao uwezo wa kuumba roho na chembechembe za ulimwangu wala hawakubali kuwa anaweza kuipa roho yoyote wokovu wa milele.<sup>35</sup> Kadhalika mapadri nao hawamtambui

---

<sup>35</sup> Ni mahali pa kushukuru kuwa Mungu wetu daima hutuonyesha mifano ya uwezo wake ili imani yetu isitawi. Kwa mfano kabla ya tetemeko la tarehe 4 April 1905, mara nne katika nyakati mbai mbali aliniarifu kwa wahyi wake kuwa tetemeko kali sana litatokea Punjab, nalo tetemeko hilo kali likatokea kweli asubuhi ya Jumanne, tarehe 4 Aprili 1905 na ilikuwa msimu wa rabi.\* Na Mwenyezi Mungu Mweza Akaniarifu tena kwamba katika msimu wa rabi matetemeko makali sana yatatokea tena. Basi tarehe 28 Februari 1906, katika msimu wa rabi, tetemeko kali sana likatokea. Katia mlima wa Mansuri tetemeko lilikuwa kali mpaka watu wakapotewa na fahamu. Na katika siku hizo hizo kule Marekani pia tetemeko likatokea lililokuwa kali sana mpaka miji kadha ikaangamia. Hivyo basi, Mungu wa kweli ndiye yule Mungu ambaye hata siku hizi pia Anatudhihirishia kudra

## Chemchem ya Ukristo

---

Mungu kuwa Mweza. Kwani, Mungu wao aliendelea kupigwa na wapinzani wake, akatiwa gerezani, akachapwa mijeledi, katundikwa msalabani. Kama angekuwa Mweza asingedhalilika kiasi hiki juu ya kuwa Mungu. Na tena kama angekuwa Mweza angekuwa na haja gani ya kufikiria kuwa afe mwenyewe ili watu wapate kuokoka kwa njia hii. Yule mtu ambaye akiwa Mungu akawa mfu kwa muda wa siku tatu, ni aibu hata kutajia uwezo wake. Na ni jambo la ajabu kwamba Mungu aliendelea kuwa mfu kwa siku tatu, lakini watu wake wakakaa hai siku tatu bila Mungu.

Na hali ya imani ya watu hao katika tauhidi (Umoja wa Mwenyezi Mungu) ndiyo kuwa Maarya wanamshirikisha Parmeshar na chembechembe zote na roho zote katika kuwepo kwa hizo zenyewe na wanasibisha kuwepo kwao na kubaki kwao kwa nguvu na uwezo wa vitu hivyo. Na huu ndio ushirikina mtupu.

---

zake zilizo hai, kwa njia ya wahyi wake. Na kuna maelfu ya matabiri yaliyotokea sawa na wahyi wa Mungu niliofunuliwa. Mwandishi.

\* Katika bara Hindi Rabiuni ni majira baina ya kipupwe na kiangazi. Kipupwe kinapokurubia malizika rabiuni inaanza kabla hakijaingia kiangazi. Mwenezi.

Ama Wakristo, basi, hali yao ni kuwa wana itikadi kinyume kabisa na tauhidi.<sup>36</sup> Yaani, hao wanaamini miungu watatu, yaani, baba, mwana na roho mtakatifu. Na jibu lao hili ni la kipuuzi kwamba sisi tunawatambua watatu kuwa mmoja. Jibu hilo la kipuuzi hakuna mtu mwenye akili anayeweza kulikubali. Kama miungu hao watatu, kila mmoja wao anakuwepo peke yake kwa kujitegemea na kila mmoja wao peke yake ni

---

<sup>36</sup> Itikadi iliyoifundisha Kurani Tukufu ni kuwa vile Mungu Alivyoziumba roho, ndivyo Alivyo na uwezo wa kuziondoa pia. Na roho ya mwanadamu hupata uzima wa milele kwa upaji wake na fadhili zake si kwa uwezo wake binafsi. Ndiyo maana, watu wanaompeda na kumtii Mungu wao kikamilifu, na kwa ukweli na uaminifu huanguka kwenye kizingiti chake, hao hasa wanajaliwa uhai mkamilifu na ndani ya hisia zao za asili hujaliwa wepesi na asili zao hujaliwa nuru ambayo kwa nuru hiyo hali ya kiroho isiyo ya kawaida huchemka ndani yao. Na nguvu zote za kiroho walizokuwa nazo duniani hupanuliwa baada ya kifo. Tena baada ya kufa, kwa mnasaba walio nao na Mtukufu Mwenye heshima hunyanyuliwa mbinguni na hiyo yaitwa Rafa' (kunyanyuliwa) katika istilahi ya Sheria. Lakini wale wasiokuwa waaminio nao hawana uhusiano safi na Mwenyezi Mungu, hao hawajaliwi uhai huo na wala sifa hizo hawazipati, kwa hiyo watu hao huhesabiwa kuwa wafu. Basi, kama Mwenyezi Mungu Asingekuwa Muumba wa roho, yeye asingeweza kuonyesha tofauti hiyo baina ya mwaminio na asiye kuwa mwaminio kwa mamlaka yake yenye uwezo. Mwandishi.

## Chemchem ya Ukristo

---

Mungu mkamilifu, basi, ni hesabu gani hiyo ambayo yaweza kuwafanya hao kuwa mmoja. Hesabu ya namna hii inafundishwa ndani ya shule na chuo gani? Je, elimu yoyote ya mantiki au falsafa inaweza kueleweshwa kuwa hao watatu wajitegemeao wamekuwaje mmoja! Na kama mkisema hiyo ni siri ambayo akili ya mtu haiwezi kuelewa, basi huku ni kudanganya. Kwani, akili ya mtu inajua vizuri kuwa kama watatu wahesabiwe kuwa ni miungu watatu wakamilifu, hapo watatu wakamilifu kwa vyovyote vile watahesabiwa kuwa watatu siyo mmoja. Itikadi hii ya utatu siyo tu inakataliwa na Kurani Tukufu, bali inapingwa pia na Torati. Maana, katika Torati ile aliyopewa Musa hamkuelezwa chochote kuhusu utatu huo, hata hamna dokezo. Waila ni dhahiri kuwa hata kama ndani ya Torati pia kungekuweko na mafundisho yanayohusu miungu hao isingewezekana kamwe Mayahudi wayasahau mafundisho hayo. Kwani kwanza Mayahudi walisisitiziwa sana kuyakumbuka mafundisho ya umoja wa Mungu mpaka wakaamriwa kuwa kila Myahudi ayahifadhi mafundisho hayo moyoni, ayaandike kwenye miimo ya milango yake na kuwafundisha watoto wao. Aidha, kwa

kukumbusha mafundisho hayo ya Umoja wa Mungu manabii wa Mwenyezi Mungu walifululiza kutokea kati ya Mayahudi na kufundisha mafundisho hayo hayo. Hivyo, jambo hili halikuwezekana kabisa na ilikuwa muhali kuwa baada ya kusisitiziwa na kufululiza manabii, Mayahudi wangesahau fundisho la Utatu na badala yake wangeandika ndani ya vitabu vyao mafundisho ya Umoja na wangepfundisha watoto wao hayo hayo, na manabii mamia waliokuja nao wangeendelea kuwakumbusha mafundisho hayo. Wazo hilo ni kunyume cha akili. Kuhusu hiyo mimi mwenyewe nilijitahidi sana kuwadadisi Mayahudi kwa viapo kuwa ndani ya Torati nyinyi mlipewa mafundisho gani kumhusu Mwenyezi Mungu? Je, mlifundishwa Utatu au fundisho jingine? Mayahudi hao wakaniandikia barua ambazo zipo kwangu mpaka sasa. Wakaeleza katika barua hizo kuwa ndani ya Torati kamwe hamna hata dokezo la fundisho la Utatu; bali mafundisho ya Torati kumhusu Mwenyezi ni yale yale ambayo ndiyo mafundisho ya Kurani. Hivyo, twawasikitikia watu hao wanaong'ang'ania itikadi ambayo haikufundishwa ndani ya Torati wala ndani ya Kurani Tukufu.

Bali, ukweli ndio kuwa fundisho la utatu halimo hata ndani ya Injili pia. Ndani ya Injili pale palipoelezwa mafundisho, hapo pote hapana hata dokezo kuhusu utatu, bali yafundisha kumhusu Mungu mmoja asiye na mshirika. Hivyo, Mapadri wakubwa wakubwa wapinzani wamelazimika kukubali kuwa hamna fundisho la utatu ndani ya Injili. Sasa litazuka swali kuwa itikadi ya utatu imeingiaje ndani ya dini ya Kikristo? Watafiti wa Kikristo wamejibu swali hili kuwa utatu huu umetokana na itikadi za Kiyunani. Wayunani walikuwa wanaamini Madevta (miungu) matatu kama vile Wahindu wanavyoamini Trimurti (masanamu matatu). Na Paulo alipowaendea Wayahudi,<sup>37</sup> na kwa vile yeye alitaka awaingize Wayunani kwa njia yoyote ndani ya Ukristo, ndiyo maana kwa kuwafurahisha Wayunani akaingiza katika dini hii fundisho la nafsi tatu za Mungu badala ya Madevta matatu. Waila Yesu hata hakujua nafsi za Mungu ni kitu gani? Mafundisho yake kumhusu Mwenyezi Mungu yalikuwa mafundisho ya kawaida kama mafundisho ya manabii wengine kuwa Mungu ni

---

<sup>37</sup> Kwa kosa la chapa imepata kuandikwa 'Wayahudi' badala ya 'Wayunani'. Mwenezi.

mmoja, Hana mshirika. Hivyo ikumbukwe kuwa dini inayojulikana kwa jina la Ukristo, kwa kweli ni dini ya Ki-Paulo, wala si ya Kikristo, maana Yesu hakufundisha popote Utatu, na mpaka alipoishi aliendelea kufundisha kuwa Mungu ni mmoja asiye na mshirika. Na baada ya kufariki kwake nduguye Yakobo pia, aliyeshika mahali pake naye alikuwa mja mtawa, aliendelea kufundisha Umoja wa Mungu. Na Paulo akaanza kupingana na mtawa huyu bila sababu yoyote na akaanza kufundisha kinyume na itikadi zake sahihi na hatimaye Paulo akapitiliza katika mawazo yake mpaka akaanzisha dini mpya, akawatenganisha kabisa wafuasi wake na ufuasi wa Torati, na akafundisha kuwa ndani ya dini ya Kikristo baada ya kafara ya Yesu sheria haihitajiki na damu ya Yesu inatosha kuondoa dhambi, hakuna haja ya kuifuata Torati. Aidha, akatia uchafu mwingine ndani ya dini hii kwamba akawahalalishia kula nguruwe ilhali Yesu amesema ndani ya Injili kuwa nguruwe ni mchafu. Ndiyo maana katika Injili mna kauli yake kuwa msiwatupie nguruwe lulu zenu. Basi, Yesu alipoyaita mafundisho matakatifu kuwa lulu, hapo inaonekana wazi kuwa akamwita mchafu kuwa

nguruwe. Hakika yenyewe ni kuwa Wayunani walikuwa wakila nguruwe kama vile siku hizi watu wote wa Ulaya wanavyokuwa nguruwe. Kwa hiyo, ili kuwapendeza Wayunani, Paulo akawahalalishia nguruwe wafuasi wake, ilhali imeandikwa ndani ya Torati kuwa nguruwe ni haramu kwa kudumu na haijuzu hata kungusa. Ilmuradi, maovu yote yalizuka ndani ya dini hii kwa sababu ya Paulo. Yesu alikuwa mtu mnyenyekevu sana ambaye hakutaka hata mtu amwite mwema, lakini Paulo akamfanya kuwa Mungu, kama ilivyoandikwa ndani ya Injili kuwa mtu fulani alisema kwa Yesu 'Ewe Mwalimu mwema', yeye akamwambia mbona unaiita mwema. Maneno yaliyotoka midomoni mwake wakati alipowambwa msalabani yanahakikisha vizuri sana Umoja wa Mungu; maana, akasema kwa unyenyekevu kuwa 'Eloi, Eloi, lama sabakthani?' yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Je, mtu anayemwita Mungu kwa unyenyekevu hivyo na anakiri kuwa Mungu ni Mola wangu, anaweza kudhaniwa na mtu yeyote mwenye akili kuwa kweli aliwahi kudai Uungu? Ukweli ndio huu kuwa wale watu walio na uhusiano wa dhati na Mwenyezi Mungu, mara



## Chemchem ya Ukristo

---

nyingi Mwenyezi Mungu Anawafanya waseme kiistiara maneno kujihusu wenyewe ambayo kutokana na hayo wajinga wanataka kuthibitisha Uungu wao. Kunihusu mimi maneno mengi zaidi kama hayo yamesemwa kuliko Yesu,<sup>38</sup> kama vile Mwenyezi Mungu Anavyosema akiniambia:

يَا قَمَرُ يَا شَمْسُ أَنْتِ مِنِّي وَ أَنَا مِنْكَ

Yaani 'Ee Mwezi, ee Jua, wewe unatokana nami, na mimi natokana nawe.' Sasa maneno hayo, mtu aweza kuyafasiri apendavyo, lakini maana yake halisi ni kuwa kwanza Mungu Akanifanya Mwezi, maana, kama mwezi nimetoka kutoka ndani ya Huyu jua la kweli, kisha Yeye Akawa Mwezi,

---

<sup>38</sup> Safari moja niliona katika kashfi kuwa mimi nimeumba ardhi mpya na mbingu mpya, kisha nikasema hebu sasa na tumbe mtu. Hapo masheikh wasiolewa wakapiga kelele kuwa angalieni, sasa mtu huyu amedai Uungu, ilhali kashfi hii ilimaanisha kwamba kwa mkono wangu Mungu Ataleta mabadiliko makubwa kana kwamba mbingu na ardhi zitakuwa mpya, na watu wa kweli watazaliwa. Kadhalika, safari moja Mungu Akasema na kuniambia kuwa:

أَنْتِ مِنِّي بِمَنْزِلَةٍ أَوْ لَدَيْ أَنْتِ مِنِّي بِمَنْزِلَةٍ لَا يَعْلَمُهَا الْخَلْقُ

Yaani, U kwangu kama wazao na una uhusiano nani ambao dunia haiutambui. Ndipo masheikh wakawa wenye kiruu kwa hasira kuwa sasa kuna shaka gani katika kufuru, na wakaisahau aya hii: فَادْكُرُوا اللَّهَ كَدِكْرِكُمْ آبَاءَكُمْ [Basi mkumbukeni Mungu kama mnavyowakumbuka baba zenu — Mwenezi] Mwandishi.

kwani kwa njia yangu mwanga wa jalali yake ukadhihirika na utadhihirika. Yakobo, nduguye Yesu, aliyekuwa mwana wa Mariamu, kwa kweli alikuwa mtu mkweli, yeye alifuata Torati katika mambo yote na alimwamini Mungu Mmoja Asiye na mshirika na alijua kuwa nguruwe ni haramu, naye kama Mayahudi alikuwa anasali akielekea Nyumba Takatifu (Hekalu) na kama ilivyopaswa akajijua yu Myahudi, ila tu aliuamini unabii wa Yesu. Lakini, Paulo akawafanya watu walichukie Hekalu. Hatimaye ghera ya Mwenyezi Mungu ikamshika na mfalme mmoja akamuua kwa kumuwamba msalabani, na huu ndio ukawa mwisho wake. Kwa vile Yesu alikuwa mkweli na alitoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa hiyo aliepushwa na kifo cha msalabani, na Mwenyezi Mungu Akamsalimisha msalabani akiwa hai lakini kwa vile Paulo alikuwa ameuacha ukweli, kwa hiyo alikufa kwa kutundikwa mtini.

Ikumbukwe kuwa katika uhai wa Yesu, Paulo alikuwa adui wake mkali. Na baada ya kifo cha Yesu, kama ilivyoandikwa ndani ya historia ya Mayahudi, sababu ya Paulo kujiunga katika Ukristo ilikuwa ni kutafuta maslahi yake binafsi, ambyo hakuyapata kwa Mayahudi. Hivyo basi,

yeye aliingia Ukristo ili awalettee vurugu, na akajisingizia kwamba Yesu alionana nami katika kashfi na mimi nimemwamini. Na mara ya kwanza mbegu mbaya ya Utatu aliipanda Paulo huko Dimashki, na utatu huu wa ki-Paulo ulianza huko huko Dimashki. Ndiko Hadithi za Mtume s.a.w. zinakoashiria kuwa Bwana Yesu atakayekuja atashukia upande wa mashariki wa Dimashki, yaani kwa ujaji wake, utatu utafikia mwisho wake, na mioyo ya watu itaendelea kuelekea Tauhidi. Na Bwana Yesu kushukia upande wa mashariki kunaashiria ushindi wake, maana, mwanga unapodhihiri, unalishinda giza.<sup>39</sup>

Ni wazi kabisa kuwa kama baada ya Yesu, Paulo alikuwa aje kama nabii, kama ilivyodhaniwa, hapo lazima Yesu angetoa habari yake, hususan ilikuwa lazima sana kutoa habari hii kwa vile katika zama zote za uhai wa Yesu, Paulo alimpinga Yesu vikali, na alipanga njama nyingi za kumtesa. Basi, baada ya kufariki kwake, mtu huyu awezaje kuhesabiwa mwaminifu isipokuwa tu kama iwepo

---

<sup>39</sup> Ikumbukwe kuwa Qadian ambayo ndiyo makazi yangu, ipo kabisa upande wa mashariki ya Dimashki. Hivyo basi, leo bishara ile imetimia aliyokuwa ametoa Mtume Mtukufu s.a.w. Mwandishi.

bishara ya wazi ya Yesu mwenyewe kumhusu yeye na ielezwe wazi wazi ndani yake kuwa ingawa katika uhai wangu Paulo alikuwa mpinzani wangu mkubwa na aliendelea kunitesa sana, lakini baada yangu, yeye atakuwa mtume wa Mwenyezi Mungu na mtu mtakatifu sana, hususan kwa vile Paulo alikuwa mtu aliyetoa mafundisho yake mapya kinyume na mafunsisho ya Torati ya Musa a.s. Akahalalisha nguruwe. Katika Torati desturi ya tohara ilitiliwa mkazo sana, na manabii wote walitahiriwa, na Yesu mwenyewe alitahiriwa, kaifuta amri ile ya zamani ya Mungu; na mahali pa Tauhidi ya Torati akaimarisha Utatu. Akaagiza kuwa siyo lazima kutekeleza amri za Torati, na akatengana na Hekalu. Basi kumhusu mtu wa namna hii aliyevuruga vibaya sheria ya Musa lazima kungekuwa na bishara. Basi, kama hakuna ndani ya Injili habari iiyomhusu Paulo kuwa mtume, na unathibitika uadui wake kwa Yesu, naye Yu mpinzani mkubwa wa amri za kudumu za Torati, kwa nini, basi, amefanywa kiongozi wa dini? Je, kuna dalili yoyote juu ya hilo?

Kisha baada ya kupata ujuzi, jambo la lazima kwa kupata wokovu ni mapenzi ya Mungu. Jambo hili

liko wazi kabisa na halikaniki kuwa mtu hapendi kumwadhibu anayempenda, bali mapenzi huvutia mapenzi na huvutia kwake. Yule ampendaye mwingine kwa moyo apaswa kuwa na yakini kuwa hata yule anayependwa hawezi kumfanyia uadui. Bali hata kama mtu asimwabile yule anayempenda kwa moyo kuhusu upendo wake huo, hata hivyo lazima kwa athari yake mtu huyu hawezi kumfanyia uadui. Kwa sababu hiyo ikasemwa kuwa moyo huvutia moyo. Manabii wa Mungu na Mitume wake huwa na nguvu ya kavutia, basi maelfu ya watu wanavutika kwao na wanawapenda mpaka wanataka kujitolea uhai wao kwao. Sababu yake ndiyo hii hii kuwa ndani ya mioyo yao huwa wema na huruma kwa ajili ya wanadamu, hata kwamba wanawapenda watu kuliko apendavyo mama, na wanapenda raha yao hata wakijitia katika shida na taabu. Hatimaye juhudi zao za kweli zanza kuvutia kwao nyoyo njema. Na kama mwanadamu — japo si mjuzi wa mambo ya ghaibu — anapata kutambua upendo uliofichika wa mtu mwingine, basi yawezekanaje Mwenyezi Mungu Aliye Mjuzi wa mambo ya ghaibu asiwe na habari za upendo halisi wa mtu? Upendo (wa Mungu) ni kitu cha ajabu, moto wake

huunguza moto wa dhambi na huteketeza kabisa mwako wa maasi. Adhabu haiwezi kuwa pale palipo Mapenzi ya Kweli ya dhata yaliyokamilika. Na miongoni mwa alama za mapenzi ya kweli mojawapo ni hii pia kuwa katika tabia ya asili ya apendaye huimarika hofu nyingi isije uhusiano wake na mpendwa wake ukakatika, akikosea kidogo mno hujifikiria ameangamia, na hufikiria ni sumu kwake kuhitilafiana na mpendwa wake. Na huwa na hamu kubwa sana ya kumkurubia mpendwa wake; umbali na mpendwa wake humhuziunisha sana kana kwamba anajifia. Hivyo, hayafikiri mambo haya tu kuwa ni dhambi wanayoelewa watu wa kawaida kuwa usiue, usimwage damu, usizini, usiibe, usitoe ushahidi wa uongo, bali yeye huona ni dhambi kubwa hata kughafilika kidogo sana na kuelekea kwa mwingine kwa kumwacha Mungu. Kwa hiyo, yeye hufululiza kumwomba ghofira mpendwa wake wa kudumu. Na kwa vile tabia yake hairidhiki kuwa wakati wowote akae mbali na Mwenyezi Mungu, hivyo, kwa sababu ya kuwa binadamu, akipata kughafilika kidogo tu huichukulia kuwa ni dhambi kubwa kama mlima. Hii ndiyo siri kuwa wenye kuhusiana na

## Chemchem ya Ukristo

---

Mwenyezi Mungu, kwa uhusiano mtakatifu na mkamilifu, daima hushughulikia kuomba ghofira, kwani hali ya upendo ni kuwa mwenye upendo wa kweli daima huchelea isije mpenzi wake akamkasirikia. Na kwa vile ndani ya moyo wake hutiliwa kiu kwamba Mwenyezi Mungu Amridhie kikamilifu, hivyo, hata kama Mwenyezi Mungu akimwambia nimekuridhia, yeye hawezi kutulia kwa kiasi hicho. Kwani, kama ilivyo katika mahafili ya mvinyo kwamba mlevi kila mara akinywa huomba mara nyingine, ndivyo ambavyo chemchemi ya mapenzi inapochemka ndani ya mtu, mapenzi hayo hukazania kwamba radhi ya Mwenyezi Mungu ipatikane zaidi sana mpaka kipeo cha mwisho. Hivyo, kwa sababu ya upendo mwingi istighfaar pia huwa nyingi. Ndiyo maana, wampendao Mungu kikamilifu hushughulikia kuomba ghofira kila wakati na kila saa. Na alama kubwa zaidi ya maasumu ndiyo kuwa yeye adumu kushughulikia kuomba ghofira zaidi kuliko wote. Na maana ya kweli ya istighfaar (kuomba ghofira) ni hii kuwa kila kosa na kasoro inayoweza kutokea kwa mtu kwa sababu ya udhaifu wa kibinadamu, msaada uombwe kwa Mungu kwa kuondoa udhaifu huo ili kwa fadhili za Mungu

udhaifu huo usitokee na uwe umefichikana. Kisha baada ya hapo maana ya istighfaar ikapanuliwa kwa watu wa kawaida. Na hii pia ikaingia katika istighfaar kuwa kosa na kasoro iliyokwisha tokea, Mwenyezi Mungu alinde na matokeo yake mabaya na athari zake zenye sumu katika dunia na akhera. Basi, chemchemi ya wokovu wa kweli ni kumpenda Mungu Mwenye shani kidhati ambako kwa unyeneykevu na istighfaar ya kudumu kwavutia mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Na mtu anapoyafikisha mapenzi yake kwenye upeo wake na huziunguza tamaa zake za nafsi, ndipo mara moja mfano wa mwako wa moto, mapenzi ya Mwenyezi Mungu ambayo Mwenyezi Mungu anakuwa naye huangakia moyoni mwake na kumtoa katika machafu ya maisha duni, na takaso la utakatifu wa Mungu Mzima wa milele na Mhifadhi wa milele hutapakaa nafsini mwake, bali huwa anazipata sehemu za sifa zote za kiungu kwa njia ya kivuli, ndipo yeye anakuwa dhihirisho la utukufu wa Mungu, na chochote kilichofichika ndani ya hazina ya milele ya Mola Mlezi hudhihirika siri zake duniani kwa njia yake. Kwa vile Mungu Aliyeiumba dunia hii si bahili, bali neema zake ni za kudumu, na majina yake na sifa



zake haziwezi kutanguka kamwe, hivyo, kwa sharti ya kumcha Mungu na kutia juhudi Anawapatia wanaokuja baadaye chochote walichopewa watu wa awali, kama Alivyofundisha Mwenyewe ndani ya Kurani Tukufu dua hii:

إِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ۝ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ<sup>40</sup>

Yaani, Ee Mungu wetu, tuongoze njia iliyonyooka, njia ya wale waliojaliwa neema na fadhili zako. Aya hii inamaanisha kuwa fadhili na neema zilizowafikia manabii na masiddiki wote hapo kabla, utujalie hizo na sisi pia, na usitunyime fadhili yoyote. Aya hii inawapa tumaini kwamba watu wa umati huu ambamo nyimati zilizopita hazikushiriki. Maana, manabii wote walikuwa na sifa mbali mbali, nao wakajaliwa fadhili na neema mbalimbali. Sasa umati huu ulifundishwa dua hii kuwa niombeni fadhili hizo mbalimbali. Ni dhahiri kuwa sifa mbali mbali zitakapokusanyika mahali pamoja, mkusanyiko huo utazidi sana kuliko sifa hizo mbalimblai zikiwa peke yao. Kwa sababu hiyo ikasemwa kuwa:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ<sup>41</sup>

---

<sup>40</sup> Al-Faatiha, 1:6,7

Yaani, kwa sababu ya sifa zenu m umati bora kuliko nyimati zote.

Sasa yapasa kujua hii pia kwamba kwa nini iliahidiwa kukusanya sifa hizi mbali mbali ndani ya umati huu? Siri iliyomo ndani yake ndiyo kuwa Mtume wetu s.a.w. amejikusanyia sifa mbali mblai, kama vile Mwenyezi Mungu Anavyosema ndani ya Kurani Tukufu:

فِيهِدُهُمْ اَقْتَدَهُ<sup>42</sup>

Yaani, uifuate miongozo yote waliyopewa manabii wote. Hivyo, ni dhahiri kuwa mtu atakayejikusanyia miongozo hiyo yote mbali mbali, yeye mtu huyo atakuwa mkusanyiko wa miongozo yote, atakuwa mbora kuliko manabii wote. Kisha mtu atakayemfuata nabii huyu mwenye kujikusanyia sifa zote, ni lazima mtu huyu vile vile awe mkusanyaji wa sifa zote hizo kwa njia ya kivuli. Basi, siri katika kufundisha dua hii iliyomo ndani ya sura Faatiha ni kwamba wakamilifu wote wa umati huu wanaomfuata nabii mwenye sifa hizo zote nao pia wawe wenye sifa zote hizo. Hivyo, ni masikitiko kwa watu

---

<sup>41</sup> Aali‘Imraan, 3:111

<sup>42</sup> Al-An‘aam, 6:91

wanaoudhania umati huu kuwa umati uliokufa. Mungu Anawafundisha dua ili wawe wenye sifa zote kamili, lakini hao wanataka wabakie wafu tu. Kwao hii ni dhambi kubwa kuwa, kwa mfano, mtu adai nafunuliwa wahyi kama vile Yesu mwana wa Mariamu.<sup>43</sup> Kwao mtu wa namna hii ni kafiri, kwani mlango wa maongezi na Mungu umefungwa mpaka siku ya kiyama. Ni ajabu sana, watu hao wanaamini kuwa hata sasa Mwenyezi Mungu Anasikia kama alivyokuwa Anasikia hapo

---

<sup>43</sup> Watu hawa wanaoitwa masheikh wanamdhihaki Sayyedi na Bwana wetu, mbora wa mitume, mbora wa manabii, Mtume Mtukufu s.a.w. wanaposema kuwa katika umati huu hakuna mtu ambaye angeweza kuja akiwa mfano wa Isa Bin Maryamu a.s., hivyo kwa kuuvunja muhuri wa Khatmi Nubuwwat, Mwenyezi Mungu wakati fulani Atamleta tena duniani Isa huyo huyo Mwisraili. Na kwa itikadi hii si tu wanafanya dhambi moja, bali wafanya dhambi mbili. 1. Moja ndiyo hii kuwa wanalazimika kuitakidi kuwa mja mmoja wa Mungu, jina lake Isa, anayelitwa Yesu kwa Kiibrania, akiifuata sheria ya Musa a.s. kwa miaka thelathini kapata ukaribu na Mungu na akapata daraja ya unabii; kinyume chake hata kama mtu akimfuata Mtume Mtukufu s.a.w. kwa miaka hamsini badala ya miaka thelathini, hata hivyo yeye hawezi kupata ile daraja, kana kwamba kwa kumfuata Mtume Mtukufu s.a.w. hakuwezi kumpatia mtu sifa yoyote nzuri.

zamani, lakini hawaamini kuwa Anaongea hata sasa kama alivyokuwa Anaongea hapo awali,

---

Hawafikirii kuwa katika hali hii ni kudanganya tu Mungu kufundisha dua hii: صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ (Al-Faatiha, 1:7) Na ndiyo itikadi yao kwamba kwa ujaji wake mara ya pili, Isa ndiye Khatam-ul-Anbiyaa na yeye ndiye Kadhi na Mwamuzi wa mwisho. Wala hawaelewi kuwa kwa bishara hii Mungu Alikusudia kuwa kama vile watakavyozaliwa katika umati huu walio mfano wa Mayahudi, ndivyo ambavyo Amlete katika umati huu mfano wa Isa a.s. pia ambaye upande mmoja awe mwana-umati na upande wa pili awe nabii. Isa Bin Maryamu a.s., hawezi kujikusanyia majina hayo mawili. Kwani mwana-umati ni yule ambaye anapata ukamilifu kwa kumfuata tu nabii mfuatwa, lakini Isa a.s. alishapata ukamilifu hapo kabla. 2. Na dhambi ya pili ya hao watu ni hii kuwa kinyume na maneno bayana ya Kurani Tukufu wanamdhania Isa a.s. kuwa hai. Ndani ya Kurani Tukufu mna aya hii wazi wazi: فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنْتُ أَنْتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ (Al-Maaida, 5:118) Na watu hao wanafasiri Aya hii hivi kuwa 'wewe uliponiinua mbinguni pamoja na mwili wangu'. Hii ni lugha ya ajabu inayomuhusu Nabii Isa a.s. pekee. Ni masikitiko kuwa hawafikirii kuwa kama ilivyofafanuliwa katika Kurani Tukufu, swali hili Hadhrat Isa ataulizwa siku ya kiyama. Basi kutokana na maana hii inayochukuliwa ya neno *Mutawaffika* (nitakufisha) yalazimu kuwa Nabii Isa a.s. kabla hajafa atahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya kiama. Na mkisema kuwa aya فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي yamaanisha kuwa uliponifisha basi sikuwa na habari tena kuwa baada ya kufa kwangu umati wangu uliishika njia gani, maana hii pia kufuatana na itikadi yao inabatilika. Na kwa maana zote hizo mbili Mwenyezi Mungu Anaweza kutoa

## Chemchem ya Ukristo

---

ilhali kama hasemi katika zama hizi, basi hakuna dalili ya kuhakikisha kwamba Anasikia. Wale wanaotangua sifa za Mungu ni watu wenye bahati mbaya sana, na kwa kweli watu hao ni maadui wa Islam. Wanatoa ile maana ya Khatmi Nubuwwat inayobatilisha unabii wenyewe. Je, tunaweza kutafsiri Khatmi Nubuwwat kumaanisha kuwa baraka zote zilizotakiwa kupatikana kwa kumfuata Mtume Mtukufu s.a.w. zote hizo zimekoma, na

---

majibu ya udhuru wake batili kwamba kwa nini unasema uongo mbele yangu ukisema mimi sijui chochote, kwani ulirejea duniani mara ya pili, ukaishi duniani miaka arobaini, ukapigana vita na Manasara na ukavunja msalaba. Istoshe, kwa tafsiri hii yalazimu kuwa maadamu Hadhrat Isa alipokuwa hai, Wakristo hawakupotoka, bali wakapotoka baada ya kufa kwake. Basi hapo hao watu hawana budi kuamini kuwa mpaka sasa Wakristo wako juu ya haki, maana mpaka sasa Hadhrat Isa yungali hai huko mbinguni. Ole wenu! Jifilieni mbali kwa aibu!! Na mwishoni ikumbukwe kuwa kama mtu mmoja wa umati huu ambaye kwa kumfuata tu Mtume Mtukufu s.a.w. anapata daraja ya kupata wahyi, ufunuo na unabii, akipewa heshima ya kuitwa nabii, hapo muhuri wa unabii hauvunjiki. Maana huyo ni mmojawapo wa umati huu huu, yeye mwenyewe si chochote, na ubora wake ndio ubora wa nabii ambaye yeye anamfuata. Naye hawezi kuitwa nabii tu, bali ni nabii na pia mwana-umati. Lakini kuja mara ya pili kwa nabii Isa asiyekuwa mwana-umati ni kinyume cha muhuri wa unabii. Mwandishi.

sasa utashi wa kuongea na Mwenyezi Mungu ni bure tu.<sup>44</sup> لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ Je, watu hao wanaweza kutuambia kuwa katika hali hii kufuata Mtume Mtukufu s.a.w. kulifaa nini? Watu ambao mikononi mwao hamna kitu ila visa vya zamani tu, dini yao imekufa na mlango wa kupata utambuzi wa Mungu umefungwa kwao. Lakini Islam ni dini iliyo hai. Na ndani ya Kurani Tukufu katika sura Al Faatiha Mwenyezi Mungu Anawafanya Waislamu kuwa warithi wa manabii na Anawafundisha dua kuwa waombe zile neema walizopewa Manabii wa zamani. Lakini yule ambaye mkononi mwake mna visa tu anawezaje kuitwa mrithi? Ni masikitiko kwa watu waliofunguliwa chemchemi ya baraka zote, lakini hawataki kunywa hata fundu moja kutoka humo. Sasa tukirejea tena kwenye mazungumzo yetu ya awali, tunaandika kuwa chemchemi ya wokovu kama tulivyokwisha andika hapo awali, ni mapenzi na utambuzi. Na utambuzi ndio ambao kadri unavyozidi huo ndiyvo mapenzi nayo huzidi kiasi hicho, kwani sababu ya mapenzi kuchemka ni uzuri au hisani. Vitu hivyo viwili ndivyo vinavyosababisha mapenzi yachemke. Hivyo basi,

---

<sup>44</sup> Laana ya Mungu iwe juu ya waongo.

## Chemchem ya Ukristo

---

mtu anapojua uzuri na hisani ya Mwneyezi Mungu, na anapokwishashuhudia jambo hili kuwa Mungu wetu Yu Mzuri namna gani kwa sifa zake zisizo na mipaka na tena kwamba namna gani hisani zake zinatuzunguka, hapo baada ya kujua hayo mapenzi yaliyomo ndani ya asili yake tangu azali, kitabia huchemka. Na kama vile Mwenyezi Mungu Alivyo na uzuri uliokamilika kuliko wote na kufanya hisani na kubariki kwa kufululiza, ndivyo ambavyo mtu anayemtafuta Yeye, baada ya kuzitambuza sifa hizo huanza kumpenda kiasi hiki kwamba yeye hamfikirii yeyote kuwa sawa naye.<sup>45</sup> Ndipo yeye si kwa ulimi tu, bali kwa

---

<sup>45</sup> Kama tulivyokwisha andika mara kwa mara, utambuzi kamili wa Mungu hauwizi kupatikana bila wahyi wa Mungu, na maongezi na Mungu, na ishara tukufu zinazodhihiri kwa njia ya wahyi wa Mungu na kuhakikisha kudra ya Allah iliyo alama dhahiri ya Uungu wake na nguvu yake. Ni utambuzi huo ambao watafuta haki wanakuwa na njaa na kiuu yake. Huo ndio utamuzi ambao pasipo kuupata wanajifia. Basi, je, utambuzi huo haumo ndani ya Uislamu? Na je, Uislamu ni dini iliyonyauka na iliyokufa? لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ (Laana ya Mungu iwe juu ya waongo). Bali Uislam pekee ni dini iliyo hai na inampa uhai mfuasi wake, ndiyo inayotuonyesha Mungu hapa hapa duniani. Kwa baraka zake, sisi tunapokea wahyi wa Mungu, na kwa baraka zake ishara nyingi kubwa kubwa

## Chemchem ya Ukristo

---

kitendo pia humjua kuwa Mmoja Asiye na mshirika, na huwa mpenzi wa sifa zake njema na khulka zake. Na ingawa mbegu ya mapenzi ya Mungu ilipandwa katika tabia ya asili ya mtu, lakini utambuzi wa Mungu hunywesheleza mbegu hii. Maana, mpendwa yeyote hawezi kumvutia mwenye kumpeda bila utambuzi wake kupatikana na pasipo mng'ao wa uzuri na jamali na khulka zake na kumkurubia yeye. Na utambuzi kamili unapopatikana ndipo huwadia wakati ambapo mwako wa upendo wa Allah unaong'aa huangukia moyo wa mtu na mara moja humvutia kwa Mwenyezi Mungu. Ndipo roho ya mtu huangukia kizingiti cha mpendwa wa milele kwa unyenekevu wa kiupendo na kwa kupiga mbizi ndani ya mto wa Mungu Mmoja hutakasika na kutakata hata kwamba uchafu wote unaondoka na badiliko lenye nuru hutokea ndani yake. Ndipo roho hiyo huyachukia mambo machafu kama Mungu

---

zinadhihirika kwa njia yetu. Dini zote za dunia zimekwisha kufa, ndani ya dini hizo hamna baraka wala mwanga, kwa njia ya dini hizo hatuwezi kufanya maongezi na Mungu, kwa njia ya dini hizo hatuwezi kuona kazi za kimiujiza za Mungu. Je, yupo yeyote mwenye kushindana nasi katika baraka hizo? Mwandishi.



Anavyoyachukia, na radhi ya Mungu huwa radhi yake na ridha ya Mungu huwa ridha yake. Lakini kama tulivyokwisha andika sasa hivi, kwa mapenzi haya ya daraja ya juu kuchemka, yalazimu kuwa mtafuata Mungu apate kujua vizuri sana uzuri na hisani ya Mungu, na azingatie barabara moyoni mwake kuwa Mwenyezi Mungu anazo katika dhati yake sifa njema sana na uzuri na jamali isiyo na kikomo. Na kadhalika hisani zake ni nyingi mno, na Yuko tayari kufanya hisani kadri isiyoyumkinika zaidi ya hizo. Na ni shukurani kwa Mwenyezi Mungu kuwa nyenzo za utambuzi huo kamili umejaliwa umati huu kwa ukamilifu. Nasi katika kueleza sifa za Mwenyezi Mungu kamwe hatuoni aibu mbele yake.<sup>46</sup> Na

---

<sup>46</sup> Mkristo akisema Mungu wake zamani akawa mfu mpaka siku tatu huona aibu sana ndani kwa ndani kwa kauli yake hii na roho yake inamsuta kuwa je, Mungu naye huwa anakufa. Na aliyekufa safari moja aaminiweje kuwa hatakufa mara nyingine tena? Basi, hamna uhakikisho wa uhai wa Mungu kama huyo. Bali, pengine ameisha kufa, kwani hivi sasa hana alama za uhai wake. Yeye hawezi kuwaitikia wanaomwomba wakisema ee Mungu, ee Mungu, wala hawezi kuonyesha kazi yoyote ya kimujiza. Tambuni, basi, kwa yakini kuwa Mungu huyo amekufa na kaburi lake lipo katika mtaa wa Khan-yar mjini Srinagar. Ama Maarya, hakuna Mungu wa roho zao; hizo zipo zenyewe tu tangu azali wala hazikuumbwa. Mwandishi.

kadri uzuri unaoweza kufikiriwa, sisi tunakubali mazuri yote katika dhati na sifa za Mwenyezi Mungu. Wala hatuamini, kama Maarya, kuwa Mwenyezi Mungu hana uwezo wa kuumba roho au chembechembe yoyote ile, wala hatusemi kama hao, Mungu Apishe mbali, kuwa Yu bahili kiasi hiki kwamba hataki kumpatia yeyote wokovu wa kudumu. Wala hatusemi kuwa hana uwezo wa kutoa wokovu. Wala hatusemi kama Maarya kuwa mlango wa wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu umefungwa. Wala hatusemi kama hao kuwa Yu mwenye moyo mgumu hata kwamba hapokei toba ya mtu na kwa sababu ya dhambi moja huingiza roho yake katika mamilioni ya miili mbalimbali. Wala hatusemi kuwa yeye hana uwezo wa kupokea toba. Pia hatusemi kama Wakristo kuwa Mungu wetu ndiye mungu aliyewahi kufa zama fulani, akakamatwa na Mayahudi, akatiwa katika gereza na kisha akatundikwa msalabani, na alizaliwa kutoka tumboni mwa mwanamke mmoja, na alikuwa na ndugu zake wengine pia. Wala hatusemi kama Wakristo, Mungu Apishe mbali, kuwa yeye kwa kuondoa mzigo wa dhambi alikwenda motoni pia kwa siku tatu. Na alikuwa hawezi kuwaokoa watu wake mpaka afe

mwenyewe badala yao, na aende motoni kwa siku tatu. Wala hausemi kama wanavyosema Wakristo kuwa baada ya Mtume wetu s.a.w. muhuri umepigwa juu ya ufunuo na wahyi na sasa mlango wa maongezi na Mwenyezi Mungu umefungwa. Kwani, Mwenyezi Mungu ndani ya Sura Faatiha Anatufanya kuwa warithi wa neema mbalimbali za manabii wote, Anaufanya umati huu kuwa bora wa nyimati. Basi, bila shaka uzuri na hisani ya Mwenyezi Mungu ambayo ndiyo chemchemi ya mapenzi, tumejaliwa hadhi kubwa ya kuiamini zaidi kuliko wote. Na miongoni mwa Waislamu, watu wasioelewa na wenye bahati mbaya ndio wale wanaokataa ukamilifu wa uzuri na hisani zake. Upande mmoja hao wakiwashirikisha viumbe wake katika sifa zake mahsusi wanatia doa katika Umoja wa Mungu<sup>47</sup> na wanaugeuza

---

<sup>47</sup> Waislamu, hususan Ahli Hadith, walikuwa na madai makubwa ya kushikamana sana na tauhidi, lakini kwa bahati mbaya mithali hii inaonekana ni kweli juu yao: 'kuchuja mbu na kumeza ngamia'. Je, watu wa aina hii tunaweza kuwaita ndio wenye kuamini Umoja wa Mungu, ambao upande mmoja wanamwamini Nabii Isa a.s. kuwa mmoja asiye na mshirika kama Mungu. Yeye tu ndiye aliyepaa mbinguni na kiwiliwili chake na ndiye atakayekuja duniani siku moja na mwili wake, na ndiye aliyewaumba ndege. Makafiri kwa viapo mara kwa

mwanga wa uzuri wa Umoja wake kuwa giza kwa kumshirikisha na wengine. Na kisha upande wa pili wanafikiria wamenyimwa fadhili za kudumu za Mtume Mtukufu s.a.w. kana kwamba, Mungu Apishe mbali, Mtume Mtukufu s.a.w. siyo taa iliyo hai, bali ni taa iliyokufa ambaye kwa njia yake taa nyingine haiwazi kuwashwa. Hao wanakiri kuwa nabii Musa a.s. alikuwa taa iliyokuwa hai, ambaye kwa ufuasi wake mamia ya manabii wakawa taa, na Yesu akimfuata kwa miaka thelathini na kutekeleza maagizo ya Torati na kwa kuweka shingoni nira ya sheria ya Musa

---

mara walimwomba Mtume wetu s.a.w. upae mbinguni mbele yetu pamoja na mwili wako, nasi papo hapo tutakuamini, lakini wakajibiwa kuwa: **قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيَ هَلْ كُنْتُ إِلَّا بَشَرًا مَّرْسُومًا** (Banii Israaiil, 17:94) Yaani waambie kuwa Mungu wangu Yu Mtakatifu, Yeye havunji ahadi. Na kwa mujibu wa kauli yake siwezi kupaa mbinguni na mwili wangu, maana jambo hili ni kinyume cha ahadi ya Mungu. Kwani Yeye Anasmema kuwa: **فِيهَا تَحْيَوْنَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ** (Al-A'raaf, 7:26). **وَلَكُمُ فِي الْأَرْضِ مَسَاقِفَةٌ** (Al-A'raaf, 7:25). Sasa je, tufikirie kuwa Mungu alisahau ahadi yake hiyo Alipompeleka Hadhrat Isa mbinguni? Au je, Isa hakuwa mtu? Kama Isa amepaa mbinguni kwa mwili wake, sasa kwa mujibu wa maelezo ya Kurani Tukufu inalazimu kuwa Isa hakuwa binadamu? Na upande wa pili wanadai kuwa Waislamu wameelezea zile sifa za dajjal ambazo kwazo yeye analazimika kuwa Mungu. Tauhidi hii! na madai haya!! Ole wao!!! Mwandishi.

a.s. akajaaliwa kupata neema ya unabii. Lakini ufuasi wa Seyidna na Maulana Hadhrat Muhammad s.a.w. haukuweza kumpatia mtu yeyote neema yoyote ya kiroho. Bali upande mmoja kwa mujibu wa aya:<sup>48</sup> مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ akanyimwa kizazi cha kiume kilicho kumbukumbu lake la dhahiri, na upande wa pili akakosa kizazi cha kiroho pia ambacho kingekuwa mrithi wa sifa zake bora za kiroho, na kauli hii ya Mwenyezi Mungu:

<sup>49</sup> وَلَكِنَّ رَسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ikawa haina maana yoyote. Ni dhahiri kuwa katika lugha ya Kiarabu neno *Lakin* hutumika kwa *istidraki*, yaani kuhusu jambo ambalo halikuweza kupatikana, kueleza kupatikana kwake kwa njia nyingine. Basi, sawa na hiyo, aya hii inamaanisha kuwa Mtume Mtukufu s.a.w. hakuwa na kizazi cha kimwili cha kiume, lakini atakuwa na wazao wengi wa kiroho, naye amefanywa kuwa muhuri wa manabii, yaani hakuna sasa atakayepata cheo cha unabii pasipo muhuri wa ufuasi wake. Ilmuradi hii ndiyo iliyokuwa maana ya aya hii iliyogeuzwa na neema ya kupata unabii katika siku zijazo ikakataliwa,

---

<sup>48</sup> Al-Ahzaab, 33:41

<sup>49</sup> Al-Ahzaab, 33:41

ilhali kukataa huku kunamvunjia Mtume s.a.w. heshima na kumshushia hadhi yake kabisa. Maana, ubora wa nabii ni kuwa yeye kwa njia ya kivuli ampatie mwingine sifa za unabii na kumlelea kikamilifu katika mambo ya kiroho. Manabii huja kwa kutoa ulezi huo, na kama mama huwapakata watafutao ukweli na kuwanyonyesha maziwa ya utambuzi wa Mungu. Basi, kama Mtume s.a.w. hakuwa na maziwa hayo, Mungu Apishe mbali, Unabii wake hauwezi kuthibitika. Lakini Mwenyezi Mungu, ndani ya Kurani Tukufu, Amempa jina 'Siraj-i-Munir' (taa ing'aayo) inayowanururisha wengine na kwa kutia athari ya nuru yake huwafanya wengine wawe mfano wake. Na, Mungu Apishe mbali, kama Mtume Mtukufu s.a.w. hana baraka za kiroho, basi, kutumwa kwake duniani ni bure tu. Na upande mwingine Mwenyezi Mungu pia akawa mdanganyifu ambaye alifundisha dua hii kwamba ombeni kupata sifa za manabii, lakini moyoni katu hakuwa na nia ya kuwapatia sifa hizo, bali nia yenyewe ilikuwa kwamba watabakizwa wakiwa vipofu wa kudumu.

Lakini, enyi Waislamu, zindukeni, wazo kama hilo ni ujahili na ni ujinga mtupu. Kama Islam ni

dini iliyokufa kabisa basi ni kaumu gani mnayoweza kuiita kwayo. Je, maiti ya dini hii mtaipeleka Japani au mtaiweka mbele ya Ulaya? Na ni mjinga gani atakayeingiwa na upendo wa dini iliyokufa, isiyo na baraka na wema wa kiroho kwa kulinganisha na dini zingine za zamani. Katika dini zilizopita wanawake pia walipokea ufunuo kama vile mama yake Hadhrat Musa a.s. na Bi Maryamu r.a., lakini nyinyi juu ya kuwa wanaume hamlingani hata na wanawake hao. Bali, enyi wajinga na viofu wa macho! Mtume wetu s.a.w., Seyyidna na Maulana (maelfu ya salamu zimfikie) amewapita manabii wote kwa kutoa baraka zake nyingi, kwa sababu baraka za manabii waliopita zilifikia hatua fualni kisha zikakatika, na sasa mataifa hayo na dini hizo ni maiti, hazina uhai tena hata kidogo. Lakini baraka za Mtume Mtukufu s.a.w. za kiroho zingali zinaendelea kupatikana mpaka siku ya kiyama, ndiyo maana kwa sababu ya baraka hizi hailazimu umati huu kwamba Masihi aje kutoka nje, bali kulelewa tu chini ya kivuli cha Mtume s.a.w. kunaweza kumfanya mtu wa kawaida kuwa Masihi kama alivyonifanya mimi.

Sasa tukirudi kwenye mada yetu tunaandika kwamba njia ya wokovu iliyoieleza Islam, falsafa yake ni kuwa upande mmoja ndani ya asili ya mtu imewekwa sumu tangu azali inayoelekeza kwenye dhambi, na upande mwingine katika asili ya mtu imewekwa dawa ya kuzuia dhara ya sumu, ambayo ndiyo mapenzi ya Mungu. Tangu mwanadamu aumbwe nguvu hizo mbili zinaendelea pamoja naye. Nguvu yenye sumu inamtayarishia mtu sababu za adhabu, na nguvu ya kuzuia dhara ya sumu ambayo ni nguvu ya mapenzi ya Mungu yateketeza dhambi kama vile moto uteketezavyo takataka. Siyo katu kwamba nguvu ya dhambi ambayo ni sababu ya adhabu iliwekwa ndani ya tabia ya mwanadamu tangu azali, lakini njia ya kujiokoa katika dhambi ikazuka tangu muda mfupi tu uliopita, yaani tangu pale Yesu alipowambwa msalabani. Itikadi ya aina hii ataikubali yule tu asiye na akili timamu hata chembe katika ubonga wake, bali nguvu hizo zote mbili ilijaliwa taiba ya asili ya mtu tangu kale, tangu alipoumbwa binadamu. Siyo kwamba sababu za kutenda dhambi Aliiweka Mwenyezi Mungu ndani ya asili ya mtu tangu awali, lakini hakukumbuka katika siku za mwanzoni dawa ya



## Chemchem ya Ukristo

---

kumpatia wokovu, akaigundua baada ya miaka elfu nne.

Sasa tunafikia mwisho wa madhumuni haya, na kwa jina la Mungu tunawapeni ushauri kuwa kama mnapenda kupata baraka zilizo hai, basi msimtaje Yesu yule aliyekwisha kufa zamani, na hazipo baraka zake zilizo hai, na kaumu yake badala ya kulewa kwa mapenzi ya Mungu imewapita wote katika kulewa kwa kileo, na badala ya kujipatia mali ya kimbinguni wanayo mapenzi ya mali ya duniani, hata kama ipatikane kwa kucheza kamari. Bali yapaswa mwingie katika silsila ya Masihi wa Muhammadi amabye ndiye <sup>50</sup> إِمَامُكُمْ مِنْكُمْ na anatoa baraka papo hapo.

Sasa mnayo hiari.

Mwandishi,  
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,  
Masihi Mau'udi.

---

<sup>50</sup> Imamu wenu kutoka miongoni mwenu.  
(Sahihi Bukhari, kitabul Ambiya, Bab Nuzuli Isa)



## **Maombi mbele ya Mwenyezi Mungu *subhanahu wa taala***

(shairi la Kiajemi na mwandishi)

*Ewe ambaye kichwa changu, uhai wangu,  
moyo wangu, na kila chembe yangu  
vimejitolea kwako, kwa rehema yako  
ifungulie fuadi yangu kila mlango wa  
utambuzi wako.*

*Mwana-falsafa yu mwenda wazimu  
akutafutaye kwa akili; njia yako  
iliyofichikana i mbali na akili.*

*Miongoni mwao hakuna alijuaye Baraza  
lako; aliyepata kulijua, akalijua kwa hisani  
zako nyingi mno.*

*Unawajalia wakupendao dunia zote mbili,  
lakini machoni mwa watumishi wako dunia  
zote mbili si kitu.*

*Tupa jicho la huruma mara moja ili vita na  
mapigano yakome, viumbe wanahitaji  
mvuto wa hoja zako.*

## Chemchem ya Ukristo

---

*Onyesha ishara moja ili nuru yako ing'are duniani, na ili kila mkana Islamu awe mwenye kukusifu.*

*Hata kama ardhi ikiwa chini juu sitakuwa na huzuni yoyote, huzuni yenyewe ndiyo kwamba isije njia yako ing'aayo ikapotea.*

*Midahalo na mijadala ya kidini ni bure; katisha maneno kwa kuonyesha ishara zilizo kubwa sana.*

*Kwa matetemeko utingishe tabia ya wapinzani ili wakichelea walikimbilie Baraza lako.*

*Kwa sura ya tetemeko utiririshe chemchemi ya rehema; mpaka lini ataendelea kuungua kwa huzuni mtumishi wako akuliliaye.*